# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 3 | Septemba 18, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO




# KIDONGE KICHUNGU CHA RUTO

**Rais amejua uhalisia wa mambo na ameamua kusukuma dawa chungu kwa koo za Wakenya ili kuokoa uchumi. Itabidi atafute namna ya kushughulikia masharti ya IMF na matarajio makubwa ya wafuasi wake wanaoamini ana suluhisho la gharama inayopanda ya maisha**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

# anywhere, anytime.


Follow the link to subscribe

> ***epaper.nation.africa.***

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111
Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

# Lazima serikali ichukue muda wake na kurekebisha uchumi



Mutuma Mathiu

Huku ukiwa umepondwa na matukio ya nje - Covid-19 na athari za uzalishaji, usambazaji na huduma kama utalii sawa na vita vinavyoendelea Ukraine, ambavyo vimefanya bei ya mafuta kupanda na kuvuruga ununuzi wa nafaka - na kuathiriwa na presha za kawaida za humu nchini, Kenya iko katika hali tete zaidi kuwahi kutokea kwa miaka mingi.

Mfumko, unasonga mbele kwa hatua za kasi, kila hatua ikielekeza nchi karibu na hali mbaya zaidi ya uchumi, na pengine kuvurugika kwa jamii.

Mlima wa deni la umma, linaloshangaza kwa kiwango na hali yake ikilinganishwa na enzi za Narc, kusema wazi, linatisha. Hali hiyo imharibu uwezo wa sekta ya kibinafsi wa kuunda nafasi za ajira na utajiri, inachoma uwezo wa nchi wa kutunza watu wake, inayeyusha uwezo wake wa kukabiliana na hatari za siku zijazo.

Kushuka kwa thamani ya shilingi kunazidisha tatizo la deni na kuchochea mfumko.

Serikali inayoingia mamlakani imekuwa ikilalamika vikali kuhusu jinsi hali ilivyo mbaya na jinsi Hazina ya nchi imeporwa na serikali iliyoondoka.

**Hata hivyo, ukweli mchungu ni kwamba, licha ya ubaya wa makosa yanayodaiwa kufanywa na serikali ya Kenyatta, serikali sasa ni ya Kenya Kwanza. Kazi ya meneja sio kugundua na kuripoti shinda, ni kuzitatua. Ikiwa mtu ameiba mali ya umma, wewe ndio serikali; irudishe. Ikiwa uchumi ni mbaya, urekebishe.**

Ni kweli, serikali inayoondoka ilizamisha mabilioni ya pesa katika miradi ambayo gharama yake halisi na thamani ni suala la mjadala. Ni kweli pia, kuna hatari ya uchumi kuvurugwa na ubepari. Huwezi kufanya sera nzuri za kiuchumi ukizingatia masilahi ya kibinafsi katika maamuzi hayo.

Hata hivyo, ukweli mchungu ni kuwa, hata kama makossa yanayodaiwa kufanywa ya Kenyatta ni makubwa namna gani, Kenya Kwanza ndiyo serkali sasa. Kazi ya meneja si kugundua na kuripoti shida, ni kuzitatua. Ikiwa mtu ameiba mali ya umma, wewe ndio serikali; irudishe. Kama uchumi ni mbaya, urekebishe. Sera ya uchumi haitaki vituko vingi hasa wakati wa mzozo.

Fikira thabiti, zilizokitwa katika mchakato unaolinda maamuzi kutoka vita vya maelezo, na talanta inayofaa, ndivyo vinavyohitajika. Watu werevu kama Dkt David Ndii, wanauchumi watajika na watu werevu wa kufikiria ndilo kundi linalohitajika kutoa suluhu bunifu katika hali kama hii, na kamwe hawajapungua katika serikali na wasomi.

Ni lazima serikali mpya iongoze kwa kuonyesha mfano. Ni lazima ikaze matumizi ya umma, kupunguza madeni na kuwajibikia kila shilingi. Ni vizuri kuvunja mitandao ya waporaji wa mali ya umma, lakini haitakuwa manufaa iwapo nafasi yao itachukuliwa na watu wako.


Wakati huo huo, ni lazima itakuwa vigumu kuamua kati ya kutimiza ahadi za kampeni za uchaguzi na kufufua uchumi. Ni mahali pabaya kujipata: wapiga kura wanatambua shibe; si juhudi.

Mzigo wa uongozi ni kujitoa mhanga. Lakini matunda ya usimamizi wenye nidhamu na makini bila shaka yataonekana na kila mtu mapema kabla ya hujakutana na mpiga kura katika uchaguzi mwingine.

Vinginevyo, utakuwa mashakani.

*mmutuma@ke.nationmedia.com*

# Yaliyomo




**8 UHALISIA MKALI WA MAMBO:** Ruto anakabiliwa na chaguo hatari la kisiasa la kutotimiza baadhi ya ahadi zake za kampeni za uchaguzi huku hali ya uchumi ikibainika katika serikali yake mpya.

**9 SERA YA KIGENI YA KENYA:** Kutoka SADR hadi Somalia na China, Ruto bado hajaamua jinsi ya kushughulikia uhusiano wa kigeni. Kufikia sasa, ameweza kutoa hisia mseto.

**21 NI WAKATI WA MARIDHIANO YA KITAIFA:** Uchaguzi Mkuu ukiwa umepita, tunahitaji mdahalo wa kuponya maovu ambayo yamefanya mchakato wa uchaguzi katika nchi yetu kuwa mchungu na kuzua mgawanyiko.

**22 UHASAMA WA NDUGU WANUKIA:** Vigogo wa Magharibi mwa Kenya Musalia Mudavadi na Moses Wetang'ula kila mmoja anaamini ni 'wa tatu' kisiasa na mamlaka



Darubini Ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Mutuma Mathiu** Mhariri Mkuu

**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji

**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Benjamin Situma, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

## Marais 500 na watu maarufu kumzika Malkia



Wabebaji jeneza la Malkia wakiweka jeneza la Malkia Elizabeth II kwenye jukwaa maalumu katika ukumbi wa Westminster, mnamo Septemba 14. PICHA | AFP

# Mazishi ya Malkia: Marais kutumia mabasi

Mazishi ya Malkia Elizabeth yanatarajiwa kuwa moja ya mikusanyiko mikubwa ya kifalme na kisiasa kuandaliwa Uingereza kwa miongo mingi.
Mialiko ilitumwa wiki hii, huku viongozi wa nchi 500 na watu mashuhuri kutoka nje ya nchi hiyo wakitarajiwa kuhudhuria.
Wengi wa viongozi hao wameambiwa wafike kwa ndege za kibiashara na kufahamishwa kuwa watasafiri kwa basi moja kutoka eneo moja magharibi mwa jiji la London.
Eneo la mazishi la Westminster Abbey lina uwezo wa kutoshea watu karibu 2,200.
Watu wa familia za kifalme kutoka kote Ulaya, ambao wengi wao wana uhusiano wa damu na Malkia, wanatarajiwa. Mfalme wa Ubelgiji, Philippe na mkewe, Malkia Mathilde, wamethibitisha watakuwepo, sawa na Mfalme Willem-Alexander wa Uholanzi na mkewe, Malkia Maxima, na mama yake, Beatrix, aliyekuwa Malkia wa Uholanzi.
Mfalme Felipe na Malkia Letizia wa Uhispania pia wamekubali mwaliko, sawa na familia za kifalme Norway, Uswizi, Denmark na Monaco. Ikulu ya White House imethibitisha kuwa Rais Joe Biden atahudhuria akiwa na Mama Taifa Jill Biden, ingawa inaarifiwa kuwa hawatasafiri kwa basi hadi eneo la mazishi.

## Yaondolewa katika kalenda ya mbio 2018

# Huenda F1 isirudi Malaysia hivi karibuni



Huenda mbio za Formula One zisirudi nchini Malaysia hivi karibuni huku serikali ikielekeza juhudi zake katika kujenga uchumi unaodorora kwa sababu ya janga la corona.
Azhan Shafriman Hanif, Afisa Mkuu Mtendaji wa shirika la Sepang International Circuit, lililokuwa likiandaa mbio hizo, alisema serikali huenda ikafikiria upya uamuzi wake baada ya miaka miwili au mitatu.
Shirika la Sepang, liliandaa mbio kwanza 1999, huku Grand Prix ya mwisho ikiandaliwa huko 2017. Malaysia ilijiondoa katika kalenda ya F1 kutoka 2018 kufuatia kupanda kwa gharama ya kuandaa mbio hizo. "Kwa sasa, jibu ni hapana," akasema Azhan Shafriman alipoulizwa iwapo Malaysia inapanga kuandaa mbio hizo tena.

## Njaa kali na mabadiliko ya hali ya anga

# IMF yahimiza tahadhari ya sera Afrika




Ni lazima nchi za Afrika zijitahidi huku zikiwazia mageuzi ya uchumi wakati wa hali mbaya ya njaa na mabadiliko ya hali ya anga. Katika ripoti mpya, Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF) limesema serikali za Afrika zinakabiliwa na "hali mbaya ya mazingira" katika sera ya uchumi.
"Mabadiliko ya hali ya anga na hali mbaya ya kushindwa kujitosheleza kwa chakula, itahitaji kuzingatia kwa makini sera dhidi ya matatizo ya ufadhili na uwezo," inasema ripoti hiyo.
Watu 123 milioni au asilimia 12 ya idadi ya watu katika nchi eneo la Sahara, wanatarajiwa kukosa chakula, inasema.
Athari za chumi kutokana na janga la Covid-19 zimeunganana na kupanda kwa bei za nafaka kutokana na vita nchini Ukraine, inaongeza.
Wakati huo huo, Afrika Mashariki inakumbwa na kiangazi kibaya zaidi kuwahi kuonekana katika miaka ya hivi majuzi.
Licha ya matatizo haya, mageuzi kadhaa yaliyofanywa kuweka huru biashara, kanuni na masoko yanaonekana," inasema IMF. "Uhuru wa kibiashara na kuagiza bidhaa tofauti kutoka nje, kunaweza kuimarisha hali ya chakula, usambazaji na bei katika eneo hilo," shirika hilo lilipendekeza.
Lilitoa mfano wa Zambia kuzuia mahindi yake kuuzwa nje mnamo 2020. Kama baadhi ya mavuno yangepatikana, huenda yangesaidia kukabiliana na uhaba wa chakula kusini mwa Afrika.
IMF ilifufua ahadi yake ya kusaidia nchi za Afrika zinazohitaji msaada wa kiufundi na kifedha.

## Acheni vita visivyo na maana Ukraine

# Papa: Dini isitumiwe vibaya



Dini haifai kutumiwa kama nguzo ya mamlaka, Papa Francis aliambia mkutano wa dini tofauti nchini Kazakhstan.
"Tusikubali kutetea ghasia. Tusiruhusu watu wazuri watumiwe vibaya na walio waovu. Wazuri hawafai kuwa nguzo ya mamlaka, au mamlaka kuwa nguzo ya wazuri," akasema.
Aliongea siku moja baada ya kuomba amani na kukomeshwa kwa vita "visivyo na maana na hatari nchini Ukraine.
"Tukikumbuka mabaya na makosa ya siku zilizopita, tujitahidi kuhakikisha Mwenyezi hatakuwa tena mateka wa tamaa ya binadamu ya mamlaka," akasema Francis. "Tujinasue kutokana na dhana potovu zinazomchukiza Mungu."

## SAHIHISHO



Katika ukurasa wa 11 wa toleo la Septemba 11 la Daruni ya Wiki, tuliweka kimakosa picha ya aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji la Kenya, Richard A. Koske (kushoto), na kumtambua kuwa Achieng' Oneko (kulia), ambaye alikuwa Waziri wa Utangazaji. Tunaomba radhi kwa kosa hilo ambalo halikukusudiwa.




ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

■ UCHUMI HALI MAHUTUTI

# RUTO: HAKUNA NJIA YA MKATO

*Rais yumo katika hali tete huku akijaribu kufufua uchumi uliosambaratika. Huku sehemu kubwa ya ushuru ikitumika kugharamia gharama za lazima kama vile mishahara, malipo ya uzeeni na madeni, utawala mpya una nafasi finyu ya kufanyia mabadiliko mipango ya matumizi ya serikali*



**Rais Ruto atahudumu chini ya masharti magumu ya IMF, yanayomlazimu kufanya mabadiliko yasiyo maarufu kisiasa katika sekta mbalimbali.**

● NA JAINDI KISERO

Uhalisia umemlazimisha Rais William Ruto kumeza kidonge kikali cha Shirika la Fedha Ulimwenguni. Wakati wa kampeni, moja kati ya ahadi kuu alizotoa ni kupunguza gharama ya maisha kwa kushusha bei za chakula na mafuta – mambo mawili makuu mbayo yamesababisha joto na shinikizo zilizopo kwa sasa katika uchumi.

Hasa, wachanganuzi walibashiri kuwa Rais mpya angetangaza msururu wa ruzuku kukinga familia kutokana na athari kali za bei za juu za mafuta, chakula na usafiri zinazozidi kupanda na kubadilika kila mara.

Alipata ushindi wake kutokana na ushawishi wake katika majukwaa ya kampeni alikojionyesha kama kiongozi anayejali maslahi ya raia wa kawaida na mwenye suluhisho kwa kila tatizo la kiuchumi linalokumba nchi.

Wataalamu wa sera za kiuchumi walimtaja kuwa mwanasiasa anayependa kufurahisha watu wa kawaida – na msimamizi sugu wa kodi na matumizi ambaye huenda akaondoa viwango vya juu vya matumizi vilivyokuwa vimewekwa na serikali iliyoondoka ya Rais Uhuru Kenyatta.

Punde baada ya kuapishwa, Rais Ruto alishangaza wengi. Lugha yake ilibadilika. "Ni sharti tuanze kuishi kuambatana na uwezo wetu," akasema, akirudia kauli na msimamo sawa na wa serikali ya Kenyatta.

Ni tangazo la Rais Ruto kuhusu miradi ya ruzuku inayolipiwa na serikali ambayo iligonga ndi-

...Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

■ KIPINDI KIGUMU MBELE YA 'TAIFA LA MAHASLA'

# RAIS AMEBANWA NA MAMBO



Benki Kuu ya Kenya. Kutengana na Shirika la Fedha Ulimwenguni kunaweza kuvuruga nafasi za kupenya masoko ya kimataifa.

**Katika ruzuku ya mafuta pekee, mlipa ushuru ametumia jumla ya Sh144 bilioni, ambazo ni Sh60 bilioni katika miezi minne iliyopita. Mpango huo ukiendelea hadi mwisho wa mwaka wa kifedha, utagharimu mlipa ushuru Sh280 bilioni, ambazo ni sawa na bajeti nzima ya maendeleo nchini**

Rais William Ruto

...Kutoka Uk 5

po kuhusu mwelekeo wa sera ya kiuchumi ambao utafuatwa na serikali mpya. Alisema: "Katika ruzuku ya mafuta pekee, mlipa ushuru ametumia jumla ya Sh144 bilioni, ambazo ni Sh60 bilioni katika miezi minne iliyopita. Mpango huo ukiendelea hadi mwisho wa mwaka wa kifedha, utagharimu mlipa ushuru Sh280 bilioni, ambazo ni sawa na bajeti nzima ya maendeleo nchini."

Huku akikashifu serikali ya mtangulizi wake, Ruto alisema jaribio la kisiasa la serikali inayoondoka la kuweka ruzuku ya unga wa mahindi kabla ya Uchaguzi Mkuu haikufaulu. "Mpango huo ulimeza Sh7 bilioni kwa mwezi mmoja, bila matokeo yoyote," kasema.

Hatua yake ya kuondolea mbali ruzuku ya bei mafuta haukushangaza wachanganuzi wa kiuchumi. Wanaofutilia shughuli kati ya Kenya na IMF walijua kuondolewa kwa ruzuku ya mafuta kulikuwa kimoja cha vidonge vichungu chini ya mpango wa IMF na Kenya.

Katika masharti yake mapya, IMF katika moja ya nakala zilizochapishwa kwenye tovuti yake, ilishangaa kuwa ruzuku ya kila mwezi ya iliruka kutoka kiasi kidogo sana Julai 2021 hadi Sh13 bilioni kufikia Juni 2022.

Shirika hilo linaonya kuwa ruzuku ya mafuta itakuwa ghali sana na kulemea Kenya, hasa bei za mafuta kimataifa zikiendelea kupanda.

"Kudumisha bei za mafuta katika kiwango tangu Juni 2022 kutasukuma juu gharama ya ruzuku ya mafuta kwa karibu asilimia 1.9 ya mapato ya jumla ya nchi katika mwaka wa kifedha wa 2022/2023," likasema shirika hilo.

Masharti ya IMF yanahitaji Kenya ibadilishe njia za kuweka bei ya mafuta na kuteua "jopokazi la kusimamia kuondolewa kwa ruzuku ya mafuta mwaka wa sasa wa kifedha". Linataka pia serikali ihakikishe hatua za kuweka bei ya mafuta zinaambatana na vipimo vya upungufu wa bajeti vilivyokubaliwa na IMF.

Ni wazi kuwa Rais Ruto, atajipata hali tete akijaribu kufuata masharti ya IMF na matarajio makubwa ya wafuasi wake wanaoamini ana suluhisho kwa gharama ya juu ya maisha. Kama bei za mafuta katika soko la kimataifa hazitaimarika, huenda makundi ya ngome ya Rais Ruto maarufu kama "mahasla" yakaanza kulalamika na kushinikiza serikali yake kuthibitisha kuwa rais mpya anaweza kutoa mwongozo kuhusu bei za juu za mafuta na chakula.

Dalili ni kuwa huenda hali ya maisha ikawa mbaya zaidi. Bei za mafuta kimataifa zilipanda kwa zaidi ya asilimia 30 kati ya Februari na Mei, baada ya Urusi kuvamia Ukraine. Kwa sasa, makadirio ya bei katika masoko siku za usoni yanaonyesha bei za kimataifa zitaendelea kuwa juu hadi mwisho wa Disemba.


Kwa kawaida, mfumo wa Kenya wa kuweka bei za mafuta umekuwa ukimsukuma mtema nyongeza ya bei za kimataifa. Lakini serikali ya Kenyatta haikubadilisha bei za humu nchini kati ya Oktoba 2021 na Februari 2022.

Mnamo Julai, serikali iliweka ruzuku ya mafuta ambapo ada inayotozwa kampuni za kutengeza mafuta ingelipwa katika hazina iliyolengwa kukabiliana na misukosuko inayotokana na bei na gharama za kimataifa za kuagizia bidhaa nchini. Serikali ililazimika kuondoa ruzuku hiyo ili kuepuka kukiuka vipimo vya bajeti vilivyoafikiwa na IMF.

Kutokana na hali hiyo, bei za mafuta nchini ziliongezeka Machi kwa asilimia 4.1. Lakini huku bei za kimataifa zikizidi kupanda, nayo serikali ikichelewesha kulipa kampuni zina-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya Kenya




zosambaza mafuta.

Maadamu ruzuku ilikuwa imeondolewa, bei zilipandishwa kwa jumla ya asilimia 6.3 kwa mwezi Aprili, Mei na Juni.

Rais Ruto atafanya kazi chini ya masharti makali ya IMF yanayomhitaji kutekeleza mageuzi yasiyo maarufu kisiasa katika sekta mbalimbali ikiwemo kuanzishwa kwa mfumo mpana wa kodi, ukarabati wa Kenya Airways, kuimarisha mpango wa muda mrefu kifedha wa kampuni ya umeme ya Kenya Power, uchapishaji wa ukaguzi wa matumizi ya fedha za umma kuhusu matumizi ya Covid-19, uchapishaji wa umilisi muhimu wa kampuni zilizopewa kandarasi na kufanyia mageuzi mfumo wa kisheria wa kupiga vita ulanguzi wa pesa.

Ni sharti Rais Ruto atii IMF? Amechukua uongozi hazina ya serikali ikiwa hali mbaya. Huku sehemu kubwa ikiwa ya matumizi ya lazima kama vile mishahara, malipo ya uzeeni na madeni, nafasi za utawala mpya kufanya mabadiliko ya ghafla kuhusu mipango ya matumizi ya serikali ni finyu.

Utawala mpya una nafasi ndogo mno na uwezo wa kufanya jambo lolote kuu au lisilo la kawaida. Kuvunja mahusiano na IMF huenda kukatatiza, sio tu nafasi ya kupata rasilimali zaidi kutoka kwa shirika hilo bali pia kupenya katika masoko ya kimataifa.

Kufikia sasa ni dola1.2 bilioni pekee zimetolewa kati ya jumla ya dola 2.3 bilioni za Amerika chini ya mkataba ulioafikiwa kati ya serikali iliyopita na IMF.

Ingawa Kibaki alimudu kutawala kwa kujitenga na IMF, hali ilikuwa tofauti wakati huo. Alirithi uchumi uliokuwa umeathirika kwa miongo mingi ya kukosa ufadhili wa kutosha kwa miundomsingi na akaamua kufuata kinachofahamika katika vitabu vya masuala ya kiuchumi kama kanuni ya Keynesian: kopa zaidi kutoka mashirika ya humu nchini, tumia kiasi kikubwa kwa miundomsingi na udumishe viwango vya chini vya riba.

Huo ulikuwa upande wa sera ya mapato. Kuhusu sera ya kifedha, alifanikiwa kushukisha viwango vya riba kwa kutatiza mifumo katika masoko ya fedha. Katika bajeti yake ya 2003/2004, Waziri wa Fedha, David Mwiraria, alipunguza kiasi cha pesa tasilimu kutoka asilimia 10 hadi sita.

Benki zilijipata ghafla zikiwa na akiba kubwa, iliyozilazimu kuanza kuchuuza mikopo ya kibinafsi kwa wananchi. Viwango vya riba katika siku ya 91- kwenye Bili ya Hazina ya Kitaifa viliporomoka kutoka asilimia nane mnamo Disema 2002 hadi chini ya asilimia mbili mwishoni mwa 2003 na katika nusu ya kwanza ya 2004.

Biashara baina ya benki - ambapo benki hukopeshana pesa – ilitatizwa pakubwa, huku viwango vikishuka kutoka asilimia sita mwanzoni mwa Aprili 2003 hadi asilimia 0.4 katikati mwa Julai.

**Tangazo la Rais Ruto la kufutilia mbali ruzuku ya mafuta halikushangaza wachanganuzi. Wanaofuatilia kwa karibu shughuli kati ya Kenya na IMF walijua kuondolewa kwa ruzuku ya mafuta na chakula kulikuwa miongoni mwa masharti yaliyotolewa na shirika hilo chini ya mpango wake na Kenya.**

Uvurugikaji huo ulikithiri kiasi kwamba IMF ilituma upesi wajumbe, wakiongozwa na Dkt Godfrey Kalinga, raia wa Tanzania, jijini Nairobi kuonya dhidi ya tishio la kusambaratika kwa soko la dhamana na kuishauri serikali kuruhusu viwango vya riba kuanza kupanda.

Kufikia wakati Rais Kenyatta alikuwa anachukua hatamu 2013, mikakati ya kodi, matumizi na viwango vya chini vya riba ilikuwa imepitwa na wakati na haingeweza tena kuchochea ukuaji wa kudumu wa uchumi. Lakini serikali iliendelea na miundomsingi mikuu ikitumia pesa kwenye ujenzi wa barabara, bandari, reli, miundomsingi ya umeme. Tofauti ilikuwa kwamba, kinyume na enzi za Kibaki, kiasi kikubwa cha pesa zilizotumika kwa miunodmsingi kitokana na madeni kutoka nje.

Uwekezaji mkubwa kwenye miundomsingi ulikuja na haja kuu ya dola ili kufadhili uagiziaji wa vyuma na mashine kubwa kutoka mataifa ya kigeni. Mapato kutokana na majani chai, kahawa, kilimo cha mboga na maua yaliendelea kushuka. Kusambaratika kwa utalii kulizidisha masaibu ya kiuchumi nchini. Taifa liliishia kuongeza mara kwa mara kiasi cha pesa kilichotolewa kwenye akaunti za akiba na mzigo mkubwa wa kulipa madeni.

Kenya ilikuwa inatumia kiasi kikubwa cha dola kuwalipa wanakandarasi wa China na kulipa madeni ghali ya mashirika ya kifedha pamoja na Eurobonds. Kimaeneo, matokeo dhaifu kiuchumi ikilinganishwa na majirani zetu yamesababisha thamani ya pesa zao kuongezeka dhidi ya sarafu ya Kenya. Katika malengo ya wastani, taifa huenda likalazimika kuendelea kumeza tembe chungu ya IMF.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ HAKUNA SULUHU YA HARAKA KWA MATATIZO YA UCHUMI

# UHALISIA MCHUNGU WA MAMBO

*Rais anakabiliwa na hatua hatari kisiasa ya kuondolea mbali baadhi ya ahadi nyingi azotoa wakati wa kampeni baada ya serikali yake kubaini hali halisi ya uchumi wa nchi.*

● Na MACHARIA GAITHO

Hata kabla hajatulia, Rais William Ruto, amekumbana na ukweli mchungu kuwa bajeti ya kitaifa haipanuki.

Aliendesha kampeni kwa ahadi ya kumwaga pesa kwa karibu kila kundi alilolenga kuashawishi, lakini alipoapishwa kuingia ofisini Jumanne iliyopita, alikubali kuwa amerithi serikali ambayo haina pesa za kutosha kutoka kwa mtangulizi wake Uhuru Kenyatta.

Sera za 'Bottom up', zilizosisitizwa katika manifesto ya muungano wa Dkt Ruto wa Kenya Kwanza, zilipigiwa debe kuwa mageuzi ya uchumi, ambayo, kwa lugha rahisi, ni kutoa pesa kutoka kwa matajiri na kuwapa masikini ili kusaidia biashara ndogo na za kati, kuwezesha vijana na wanawake na maeneo yaliyopuuzwa na kutengwa.

Sera hiyo pia inaahdi kuongeza uwekezaji katika kilimo, hasa utoaji wa mbolea ya bei nafuu, mbegu na pembejeo zingine.

Ruto, kwa maneno yake mwenyewe, alipata shimo la kina katika Wizara ya Fedha, na sasa anakabiliwa na hatua hatari kisiasa la kufutilia mbali baadhi ya ahadi zake za kampeni, na pia kuondoa baadhi ya ruzuku ghali zilizowekwa na serikali iliyoondoka mamlakani wakati wa msimu wa kampeni. Ingawa katika kampeni Ruto alijigamba kuwa amebadilisha uchaguzi kutoka siasa za kikabila hadi siasa za masuala muhimu, itabidi akubali ukweli kuwa sera za uchumi hasa ni za kisiasa.

Kizungumkuti kichonakabili serikali mpya kilibainika siku yake ya kwanza ofisini, ilipolazimika kufanya uamuzi kuhusu ruzuku ya mafuta kabla ya mabadiliko ya bei yanayofanywa kila mwezi.

Katika hotuba yake ya kwanza baada ya kuapishwa Septemba 13, Ruto aliungama kuwa ruzuku hizo zinakausha Hazina ya Kitaifa na haziwezi kudumishwa. Alisema tayari zimegharimu serikali Sh140 bilioni, na gharama ilitarajiwa kupanda hadi Sh280 bilioni kufikia Juni mwaka ujao.

Katika kiwango cha sera, alisema ruzuku zinaweza kutumiwa vibaya, kuvuruga masoko na kusababisha mkanganyiko ambao, badala ya kuhakikisha bidhaa muhimu zinapatikana, unasababisha uhaba wake.

Alifahamu vyema kuwa serikali imekuwa ikichelewa kutimiza ahadi yake ya kurudishia pesa kampuni za kuuza mafuta, ambazo kimya kimya zilitishia kutozambaza mafuta hadi zilipwe.

Siku moja baada ya rais kuapishwa, kulikuwa na jumbe za kukanganya. Waenezaji propaganda zake katika mitandao ya kijamii walisifia ujasiri wake wa kuondoa ruzuku ambazo walidai zinafaidi kampuni kubwa za kimataifa, huku ripoti zingine zikasema ruzuku hizo zingebakia kwa angalau mwezi mmoja kusubiri mazungumzo na kampuni za kuuza mafuta. Baadaye, taarifa rasmi ilitoka kwa Mamlaka ya Kudhibiti Kawi na Petroli kuthibitisha kuondolewa kwa ruzuku kwa petroli lakini ikadumishwa kwa dizeli na mafuta taa. Kuondolewa kwa ruzuku hiyo kulisukuma bei ya petroli kutoka Sh159 hadi ya juu zaidi katika historia ya Kenya ya Sh179 kwa lita. Bei za dizeli na mafuta taa ziliongezeka kwa Sh25 na Sh20 kuuzwa kwa bei mpya ya juu ya Sh165 na Sh148 mtawalia lakini wateja bado walikingwa na ruzuku ya Sh20 na Sh26 kwa kila bidhaa.



Wakenya waliojawa na furaha wakisherehekea wakati wa kuapishwa kwa Rais William Ruto katika Uwanja wa Michezo wa Kasarani, Septemba 13. PICHA | DENNIS ONSONGO

Kutangaza mabadiliko ya sera kuhusu ruzuku lakini kuziondoa kwa baadhi ya bidhaa na kuzibakisha kwa zingine kunaweza kuonekana kukinzana, lakini ni kutambua kuwa ukweli wa kisiasa hauruhusu baadhi ya hatua.

Labda dhana katika uamuzi huo ni kuwa magari ya kibinafsi, ambayo yanatumia petroli aina ya Super, ni ya matajiri, huku mafuta taa, yakitumiwa na maskini kuwasha na kupikia nayo dizeli ikitumiwa katika uchukuzi wa umma pamoja na tingatinga na vifaa vingine vya kilimo na ujenzi.

Ni siasa pia zilizomfanya Ruto kupinga ruzuku huku wakati huo akiagiza bei ya mbolea kupunguzwa kwa asilimia 50, na asilimia inayobakia kulipwa na serikali.

Bado ni mapema na rais mpya ana watu wengi anaopaswa kufurahisha, muhimu zaidi ikiwa ni kufadhili mfumo wake wa uchumi wa 'Bottom up', ambao unaahidi kuunda 'Hazina ya Mahasla' ya kima cha Sh50 bilioni.


Anakiri kuwa mikoba ni mitupu, lakini ni lazima pesa zitoke mahali, kumaanisha zitatolewa katika bajeti zilizotengewa mambo mengine.

Serikali mpya ikikosa kabisa kabisa za kutimiza baadhi ya ahadi ilizotoa wakati wa kampeni, basi inaweza kugeuza mawazo ya Wakenya kwa kumnyooshea Uhuru Kenyatta

...Endelea Uk 11

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MALENGO YA KIMATAIFA



# SERA YA KIGENI: HUKU AU NI KULE?

*Baada ya hitilafu ya kidiplomasia kuhusu Morocco-Sahrawi na Somalia na China, Rais hajaamua jinsi kushughulikia mahusiano wa kigeni*

Na JOHN KAMAU

Umati mkubwa katika Uwanja wa Michezo wa Kasarani haukugundua hitilafu umuhimu kidiplomasia kuwepo kwa kiongozi wa kundi la Polisario Front, Rais Brahim Ghali, wakati wa sherehe ya kuapishwa kwa Rais William Ruto.

Kuwepo kwake ni ishara kuwa Kenya itaendelea kutambua eneo linalobishaniwa la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi (Sahrawi Arab Democratic Republic- (SADR) kama taifa huru wala si eneo lililojitenga kutoka Ufalme wa Morocco.

Lakini Rais Ruto alipoanza kutatambua marais wa Afrika, aliruka jina la Rais Ghali. Haijulikana hatua yakr hiyo ilikuwa kimakusudi ama ya kisiasa, lakini kilichofuatia kilionyesha kuwa Ruto hajaamua kuhusu sera yake ya uhusiano wa kigeni.

Ingawa hatuba ya rais ilikuwa na machache kuhusu sera za kigeni na mengi kuhusu masuala nchini, wachanganuzi waligundua kuwa suala la Polisario lilikuwa mojawapo la masuala muhimu siku hiyo.

Katika jukwaa la wageni mashuhuri pia aliketi Waziri wa Ujasusi wa Israeli Elazar Stern, akiwakilisha nchi yake ambayo 2020 lilitia saini mkataba na Morocco – kwa upatanisho wa aliyekuwa Rais wa Amerika Donald Trump.

Chini ya mkataba huo, Morocco ilikubali kufufua uhusiano wa kidiplmasia na Israeli, nayo Amerika ikatambua udhibiti wa Morocco wa eneo linalozozaniwa la Magharibi mwa Sahara.

Kuwepo kwa Ghali katika sherehe ya kiapo, iliyohudhuriwa na marais 17 wa mataifa ya Afrika, ilionekana kuzua hali ya mkanganyiko wa kidiplomasia.

Mnamo 1984, aliyekuwa Rais, Daniel Moi, alikabiliwa na hali sawa na hiyo akiwa Mwenyekiti wa Shirika la Umoja wa Afrika (sasa Umoja wa Afrika-AU) baada ya Polisario kualikuwa kuwa mwanachama wa 51 wa Shirika la Umoja wa Afrika (OAU). Hatua hiyo ilifanya nchi 18 kususia mkutano wa shirika hilo la bara na Morocco kujiondoa kama mwanachama.

Morocco imekuwa ikishawishi viongozi wa Afrika waiunge mkono na kutumia uwezo wake kuzalisha mbolea kwa wingi kuendeleza shughuli hiyo ya kidiplomasia.

Sahara Magharibi, ilivyojulikana awali SADR awali, na sehemu za Morocco zina asilimia 70 ya madini ya phosphate, yanayotumiwa kutengeneza mbolea yenye madini hayo.

Tangu walipokosana, Dkt Ruto na aliyekuwa Rais Uhuru Kenya, walikuwa na mitazamo tofauti kuhusu uhusiano wa kidiplomasia kati ya Kenya na SADR katika siku za usoni.

Alipokutana na balozi wa Morocco nchini Kenya mnamo Machi 2022, Ruto alionekana kupendelea mipango ya Morocco ya kudumisha uhuru wake.

Msimamo huu ulikuwa tofauti na hatua wa Kenyatta ambaye aliunga mkono Polisario, kama sehemu ya ajenda yake ya kupiganaia masilahi ya Afrika.

Haikushangaza kuwa siku mbili baada ya kuapishwa, Dkt Ruto alisema kupitia ukurasa wake rasmi wa Twitter – baada ya kupokea ujumbe katika Ikulu ya Nairobi, Kenya, kutoka kwa Mfalme Mohammed VI wa Morocco na kukutana na Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Morocco, Nasser Bourita – kuwa Kenya imebatilisha hatua yake ya "kutambua SADR na itachukua hatua za kutokomeza kabisa uwakilishi wake nchini."

Kabla ya rais kufuta ujumbe huo, tayari ulikuwa umenakiliwa na Wizara ya Masuala ya Kigeni ya Morocco, ambayo ilitangaza kuwa "kufuatia ujumbe wa Mfalme kwa rais mpya wa Jamhuri ya Kenya, Dkt William Ruto, Jamhuri ya Kenya imeamua kutotambua SADR na imeanza mpango wa kufunga uwakilishi wake jijini Nairobi.

Huku AU ikionekana kuunga mkono SADR nazo Amerika na Israeli zikiunga Morocco, inangojewa kuonekana jinsi Dkt Ruto atashughulikia masilahi ya ndani na yale ya washirika wake wa kigeni. Rais anapendelea Israeli kwa misingi ya kidini, na ilikuwa mojawapo ya nchi za kwanza kumpongeza kwa ushindi wake.

Kizungumkuti kingine kinachomkabili Ruto ni hatima ya wanajeshi wa Kenya nchini Somalia, ambako wamekuwa tangu mwaka wa 2011 pamoja na mzozo kuhusu umiliki wa eneo lenye utajiri wa mafuta ndani ya Bahari Hindi.

Inangojewa kuonekana jinsi Uhuru, ambaye amemdumishwa na Ruto kuendelea kuwa balozi wake wa amani katika ukanda huu, atakavyoshughulikia masuala ya kidiplomasia, hasa katika upembe wa Afrika. Eneo hilo limekuwa kitovu cha vita kwa miongo kadha.

Katika eneo la Afrika Mashariki, Ruto ameegemea upande wa Rais wa Uganda Yoweri Museveni. Hii ndiyo maana alikuwa wa kwanza kumtambua wa kwanza mbele ya umati katika uwanja wa Kasarani.

Uhusiano kati ya Kenya na Uganda ulikabiliwa na changamoto nyingi wakati wa uongozi wa Bw Kenyatta, ingawa nchi hizo mbili zilishikilia kuwa na uhusiano mzuri.

Uhusiano mbaya wa miaka michache iliyopita ulichangiwa na dhana kuwa Rais Museveni alikuwa akimuunga mkono Ruto. Mwaka jana, Museveni alimkaribisha Dkt Ruto nyumbani kwake eneo la Rwakitura.

Wakati wa kampeni, Ruto alionekana kushambulia China, akisema ndiyo ya kulaumiwa kwa mzigo wa madeni unaozonga Kenya. Uamuzi wake wa kuhamisha shughuli za ukaguzi wa mizigo kutoka Naivasha hadi Mombasa huenda ukaathiri mapato kutokana na uchukuzi wa mizigo kupitia reli ya kisasa (SGR) na kuchafua uhusiano kati ya Kenya na China.

Haijulikana serikali mpya ya itachukua msimamo gani ingawa Ruto alionyesha dalili alipokutana na ujumbe kutoka China majuzi, kuwa Kenya itaendelea kutegemea misaada kutoka taifa hilo ili kuendeleza miundo-msingi.

Kutoka Magharibi, Amerika imetuma Rais wa wa kampuni ya Hewlett Packard, Meg Whitman kuwa balozi wake nchini Kenya.

Hii ina maana kuwa Kenya inashikilia nafasi muhimu zaidi katika mpangilio wa masilahi ya kibiashara na kiusalama ya Amerika katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

Huku utata wa mahusiano ya kigeni ukiendelea kujitokeza, macho yote yataelekezwa kwa mtu ambaye Rais Ruto atateua kuwa Waziri wa Masuala ya Kigeni katika serikali yake mpya. Kufikia sasa ametoa ishara za kukanganya kuhusu suala hilo.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

■ DEMOKRASIA THABITI ZAIDI AFRIKA MASHARIKI



# WAKATI BORA ZAIDI KWA KENYA

*Kufuatia kuapishwa kwake, Rais Ruto sasa amepata mamlaka yote ya serikali. Anaweza kutekeleza ajenda yake barabara kwa sababu ushindi wake pia umeidhinishwa na viongozi wa ukanda wa Afrika Mashariki, bara la Afrika na dunia kwa jumla, ambao wanaonekana kuwa tayari kushirikiana na Kenya.*


● Na TONY MOCHAMA

MAGARI ya kifahari yaliyobeba marais wa mataifa ya Afrika yaliingia ndani ya Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Moi, Kasarani, asubuhi ya Septemba 13, kwa sherehe ya kuapishwa kwa Dkt William Samoei Ruto kuwa Rais wa tano wa Jamhuri ya Kenya.

Walikuwa Yoweri Museveni (Uganda), Samia Suluhu (Tanzania), Paul Kagame (Rwanda), Evariste Ndayishimiye (Burundi), Felix Tshisekedi (DRC), Ethiopia's Premier Abiy Ahmed, Somalia's Hassan Mohamud, South Sudan's Salvador Kiir, Ismail Guelleh (Djibouti), Dennis Nguesso (Congo), Lazarus Chakwera (Malawi), Emmerson Mnagangwa (Zimbabwe), Filipe Nyusi (Mozambique), Azali Assousmani wa Visiwa vya Comoros, Wavel Ramkalawan (Seychelles) na Umaro Embalo wa Guinea Bissau.

Alikuwepo pia rais wa nchi isiyotambuliwa, Jamhuri ya Saharawi, iliyo kusini mwa Morocco, eneo linalopigania kujitawala.

Mwezi mmoja uliopita, mataifa ya Magharibi, yakiongozwa na Umoja wa Ulaya (EU), yalikuwa tayari yametangaza kuwa yaliridhika na jinsi uchaguzi mkuu uliendeshwa nchini Kenya. Hii ni tofauti na chaguzi za 2017, 2013 na 2007 ambayo yalikuwa na tashwishi nazo.



Rais anayeondoka, Uhuru Kenyatta (kushoto) akimpongeza Rais William Ruto katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo Moi, Kasarani, wakati wa sherehe ya kiapo, Septemba 13. PICHA | AFP

**Mwezi mmoja uliopita, mataifa ya Magharibi, yakiongozwa na Umoja wa Ulaya (EU), yalikuwa tayari yametangaza kuwa yaliridhika na jinsi uchaguzi mkuu uliendeshwa nchini Kenya. Hii ni tofauti na chaguzi za 2017, 2013 na 2007 ambayo yalikuwa na "tashwishi kubwa nazo....."**

Taarifa ya EU kuhusu uchaguzi wa Agosti 9, 2022 ilitolewa na Balozi wa Uingereza nchini Kenya, Joseph Borell, akiwapongeza Wakenya kwa kudumisha amani wakati na baada ya chaguzi zote sita, ukiwemo wa urais.

"EU inatambua matokeo ambayo yamemwonyesha Dkt Ruto kuwa mshindi. Tunatarajia kufanya kazi naye ili kuimarisha uhusiano kati ya EU na Kenya katika nyanja mbalimbali,"

Baadaye Mahakama ya Upeo ilizima ndoto za urais za mgombeaji wa urais wa Azimio la Umoja - One Kenya, Raila Odinga, kwa kutupa malalamishi yote tisa katika kesi yake ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa urais.

Naibu Jaji Mkuu Philomena Mwilu alitaja tofauti miongoni mwa Makamishna wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) "kama vindeo, kama ndrama."

Lakini Jaji Isaac Lenaola, kwa aliyekuwa makini, ndiye aliyetangaza kifo cha kesi ya Raila alipomuuliza wakili Jothan Arwa: "Tuliwaona wateja wako (makamishna wanne wa liojitenga) wakisoma matokeo katika televisheni hadi dakika za mwisho. Je, kuna ushahidi gani wa kuonyesha kuwa hatua yao ya mkutano na vyombo wakiongozwa na Naibu

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

Mwenyekiti, Juliana Cherera, haikuwa wazo la ghafla?"

Baada ya mahakama kupuuza jambo kama lililotokana na wazo la ghafla, mlalamishi anafaa kujua ameshindwa.

Baada ya uamuzi wa Mahakama ya Upeo kutolewa, Jaji Mkuu Martha Koome alisema hadharani kwenye mazishi eneo la Meru kwamba "Kenya imepata heshima ulimwenguni kwa kuonyesha kuwa Idara ya Mahakama ni huru katika uamuzi wake.

Hata hivyo, Wakili Mkuu na Gavana wa Siaya, James Aggrey Orengo, alikataa kauli hiyo akisema uamuzi wa Mahakama ya Upeo dhidi ya mteja wake ulitokana na ushawishi wa "kisiasa".

Lakini aliyekuwa Mwanasheria Mkuu Githu Muiga naye anaiona mahakama ya sasa kuwa idara huru, ikilinganishwa na enzi za kabla ya kupitishwa kwa Katiba ya sasa mnamo 2010.

Hasa anataja enzi za utawala wa aliyekuwa Rais Daniel Moi ambapo maamuzi ya mahakama yalishawishiwa na matakwa ya Serikali Kuu.

Lakini wakili mwadilifu kama Orengo chukulia mahakama hiyo kama ambayo inaogopa kujihusisha na migogoro ya kisiasa, kama wakati wa Maraga; ambayo inazingatia zaidi idadi wala si utaratibu katika uamuzi wa kesi za kupinga matokeo ya uchaguzi wa urais.

Mwishoni mwa wiki ambayo Rais Ruto alishindi kesi katika Mahakama ya Upeo, alipata ushindi mara baada ya muungano wake wa Kenya Kwanza kunyakua viti vya Maspika wa Bunge la Kitaifa na Seneti, katika kile kilichotajwa kuwa 'Vita vya Mwisho' kati ya Kenya Kwanza na Azimio – Kenya One.

Amason Kingi, ambaye mwandishi huyu alishuhudia akizomewa na umati wa watu wakati wa kuapishwa kwa Gavana wa Kilifi, Gideon Mung'aro, alichaguliwa Spika wa Seneti.

Katika Bunge la Kitaifa, siku hiyo ya Ijumaa, aliyekuwa Seneta wa Bungoma wa Ford Kenya, Moses Wetang'ula, alishinda kiti cha Uspika wa wa Bunge la Kitaifa, licha ya kudhalilishwa vibaya na vwafuasi wa Azimio wakati wa kampeni.

Kufuatia kuapishwa kwake siku tisa baada ya uamuzi wa Mahakama ya Upeo, Rais Ruto sasa amepata mamlaka yote ya serikali.

Anaweza kutekeleza ajenda yake barabara kwa sababu ushindi wake pia umeidhinishwa na viongozi wa ukanda wa Afrika Mashariki, bara la Afrika na dunia kwa jumla, ambao wanaonekana kuwa tayari kushirikiana na Kenya.

***Mr Mochama ni mwandishi wa kitabu 'Political Party After Party: A 60-year history of political parties in Kenya.'***

> **Tunatarajia kufanya kazi pamoja kuendeleza zaidi, pamoja na serikali inayokuja ya Kenya, mashauri ya mikakati ya manufaa kwa Kenya na EU iliyoanza Juni 2021.**
>
> Balozi wa EU nchini Kenya, Josep Borell



Kutoka kushoto; Rais Yoweri Museveni (Uganda), Ismail Omar Guelleh (Djibouti) na Salva Kiir Mayardit (Sudan Kusini) waki katika Uwanja wa Michezo wa Kasarani, mnamo Septemba 13. PICHA I JEFF ANGOTE



Rais Brahim Ghali wa Jamhuri ya Sahrawi akiwa katika Uwanja wa Michezo wa Moi, Kasarani, wakati wa sherehe ya kuapishwa kwa Rais William Ruto, mnamo Septemba 13. PICHA I JEFF ANGOTE

# Ni uhalisia mkali kwa timu mpya

...Kutoka Uk 8

kidole cha lawama.

Hotuba ya Ruto haikutaja ahadi yake ya kuanzisha Tume ya Kuchunguza 'Kutekwa Kwa Serikali' chini ya utawala wa Uhuru, hatua inayonuiwa kufichua ufisadi mkubwa ambao ulinufaisha iliyokuwa familia ya Rais na washirika wao wa kibiashara.

Uchunguzi wa umma wa aina hiyo, kwa baadhi ya watu katika serikali ya Ruto, unaweza kuwa chombo kinachofaa kueleza sababu ya kutotimiza ahadi za kampeni kwa msingi kuwa serikali mpya ilirithi mikoba mitupu kufuatia miaka kumi ambayo iliporwa.

Huenda si kwa kubahatisha kwamba, aliyekuwa Mbunge wa Gatundu Kusini, Moses Kuria, mshirika wa karibu wa Ruto, tayari anatoa vidokezo vya kufichua mambo siku zijazo ambayo yatashangaza nchi. Hata hivyo, tatizo kwa Ruto ni kuwa alikuwa amefungwa kibindoni pamoja na Uhuru katika mihula miwili ya serikali ya Jubilee.

Ingawa alitengwa katika muhula wa pili baada ya Uhuru kuungana na kiongozi wa upinzani Raila Odinga, Ruto alibaki kuwa naibu rais na alifurahia minofu ya ofisi hiyo. Aidha, alitembelea sehemu kadhaa za nchi kufanya kampeni za urais ambako alijigamba kwa kila mafanikio ya serikali ya Jubilee zikiwemo barabara na miradi mingine ya miundomsingi.

Hivyo basi, Ruto anafaa kutahadhari kuanzisha uchunguzi huo ambao unaweza kumfanya atajwe kuwa mshirika-mwenza katika uporaji mkubwa.


Tofauti na baadhi ya wanasiasa wasio waangalifu katika upande wake, Ruto anafaa kuepuka kumpitisha Uhuru katika makaa ya moto ambayo yanaweza kumchoma mwenyewe iwapo uchunguzi utaonekana kuwa na nia mbaya kisiasa, jambo ambalo halijawahi kutokea Kenya ambako marais waliostaafu wanaruhusiwa kuishi kwa amani.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Habari kwa picha



Mfalme wa Uingereza Charles III akizungumza wakati wa mkutano wa Kamati ya Urithi ndani ya Ikulu ya St James, jijini London, Septemba 10, kumtangaza kuwa Mfalme mpya. PICHA | AFP




Kourtney Kardashian na mumewe Travis Barker, wakihudhuria maonyesho ya Wiki ya Mitindo Septemba 13, 2022, jijini New York. PICHA | AFP



Moshi mkubwa ukipaa angani wakati wa shambulizi la bomu la Urusi karibu na kijiji cha Hafsarja, eneo lililo chini ya utawala wa na waasi la Idlib magharibi mwa nchi mnamo Septemba 8, 2022. PICHA | AFP



Mwelekezi wa filamu Mfaransa, Alice Diop, apigwa picha baada ya kupokea tuzo la Lion of the Future (kushoto) na Silver Lion, mnamo Septemba 10, 2022, wakati wa tuzo za wanafilamu jijini Venice, Italia. PICHA | AFP



Watu waliojaribu kuingia kwa nguvu katika sherehe ya kuapishwa kwa Rais William Ruto katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Kasarani, Nairobi, Kenya, Septemba 13, 2022, wazuiawa na maafisa wa usalama. PICHA | AFP



Muigizaji wa Canada Will Amett (kushoto) amkokota mwenyeji wa televisheni Amerika, Jimmy Kimmel jukwaani walipofika kutoa tuzo katika tamasha la 74 la Emmy Awards, jijini Los Angeles, California, mnamo Septemba 12, 2022. PICHA | AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"



# NDIYE MFALME BARABARANI

*McRae Kimathi amesisimua mataifa ya Ulaya kwa ustadi wake katika mbio. Akiwa Mkenya wa kuwania Ubingwa wa mbio za magari za The FIA Junior WRC, anataka kuwa kielelezo cha vizazi vijavyo.*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

NAFASI YA VIJANA

# SIASA ZETU NI ZA KIKABILA

**MAENEO YAJIPANGA UPYA:** Japo wengi wanaamini masuala muhimu yalizingatiwa kushinda ukabila, upigaji kura na mjadala uliotawala chaguzi za majuzi ulithibitisha vinginevyo.

● NA JAMES MUGENDI



Wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu uliokamilika majuzi, wanasiasa, wachanganuzi wa kisiasa na wadadisi wengine walizungumzia jinsi suala la ukabila limepitwa na masuala muhimu. William Ruto na timu yake ya Kenya Kwanza walirudia kauli hii mara kwa mara. Lakini huu ndio ukweli halisi?

Vitendo vya wagombea wakuu wa urais, matamshi ya wanasiasa na data ya upigaji kura inaonyesha kuwa 'masuala' hayakuwa na maana yoyote ila neno la kupumbaza tu.

Bila shaka, juhudi zilikuwepo za kuangazia masuala kama vile gharama ya juu ya maisha, mapato ya kilimo, mazingira ya biashara, afya na elimu. Lakini haya yalikuwa sehemu ndogo sana ya kampeni zilizojaa propaganda za kuzua taharuki, mashambulizi dhidi ya watu binafsi na jamii tofauti kujipanga kivyake.

Wagombea wakuu wa urais walijua suala la ukabila bado ni nguzo muhimu katika chaguzi na waliweka vigogo wa jamii na maeneo katika timu zao. Ili kufanikiwa kupenya maeneo ya Magharibi na Pwani, Ruto alivutia upande wake Musalia Mudavadi na Moses Wetang'ula (Magraribi) na Salim Mvurya na Amason Kingi (Pwani) kwa kuwaahidi nyadhifa kuu katika serikali yake. Naye Raila Odinga alikuwa na Rais Uhuru Kenyatta, Martha Karua na viongozi wengine kutoka Mlima Kenya katika juhudi zake za kupata kura nyingi eneo hilo, ambalo kila mara limekuwa likimponyoka.

Odinga na Ruto walijitahidi sana kumvuta Kalonzo Musyoka, anayechukuliwa na wengi kuwa kigogo wa eneo la Ukambani. Hatimaye, Raila alifanikiwa kumshawishi pamoja na idadi kubwa ya kura za Wakamba. Ni katika eneo la Mlima Kenya pekee ambako mtindo wa kigogo wa jamii haukutumiwa.

Kenya Kwanza ilimtumia Uhuru kwa kumshutumu vikali au kumsifu kiasi kulingana na hali. Kasumba ya jitu ovu (yaani Odinga, na hivi majuzi, Uhuru), ambayo imetawala siasa za eneo hilo tangu 2013, ilitumiwa. Lakini ukabila haukuachwa nje kabisa: hatua ya Ruto kumteua Rigathi Gachagua kuwa mgombea mwenza ilichochewa sana na hili.

Licha ya hayo, Raila alipiga hatua kuu katika Eneo la Kati kupitia usaidizi wa vigogo kadhaa kutoka eneo hilo. Katika Kaunti ya Tharaka-Nithi, kwa mfano, alikopata chini ya asilimia moja mnamo 2017, Raila alipata asilimia 9.32 katika uchaguzi wa majuzi. Kwa jumla, alipata asilimia 22 ya kura katika kaunti za Mlima Kenya, zaidi ya maradufu ya alizopata katika chaguzi za 2013 na 2017.

Vivyo hivyo, kupitia Kenya Kwanza, Ruto alipata matokeo bora zaidi katika Kaunti ya Vihiga, ngome ya nyumbani ya Mudavadi, kushinda kiasi walichopata na Uhuru 2017, kiongozi huyo wa ANC alipokataliwa na wengi nyumbani kwake. Bungoma ilikuwa kilele cha kambi ya Kenya Kwanza baada ya kugeukia kabisa upande wa Ruto huku kaunti hiyo ikimuunga mkono kigogo wake, Wetang'ula. Katika Mwambao wa Pwani, Ruto alipiga hatua pia huku akipata zaidi ya kura 48,000 kushinda walizopata na Uhuru 2017.

Hivyo basi, ingawa tungetaka kuamini kuwa tumezika siasa za kikabila katika kaburi la sahau, idadi na midahalo iliyotawala kampeni ilithibitisha uhalisia tofauti.

Bw Mugendi ni mhariri msaidizi katika shirika la Nation Media Group.

*Je, wewe ni kijana mwenye maono makuu? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni na mtazamo wako kuhusu masuala ibuka kupitia baruameme*

***weeklyreview@ke.nationmedia.com***

## WANAVYOSEMA



**Kevin Lemaiyan**

Nawapongeza Wakenya kwa kudumisha amani tangu Uchaguzi Mkuu wa Agosti 9. Namhimiza rais wetu mpya awahudumie Wakenya wote kwa usawa. Sasa anatuwakilisha sote, waliompigia kura na ambao hawakumpigia. Sote tunafaa kupata mgao sawa wa rasilimali.

*- Mhasibu*



**Zemran Ahmed**

Rais William Ruto ni mtu mwenye bidii. Pia ni stadi wa mikakati na mwenye maono, kiongozi ambaye hasa Kenya inahitaji ili kusonga mbele. Uongozi utabadilisha taifa. Amethibitisha inawezekana kuinuka kutoka hali ya uchochole hadi ofisi kuu zaidi nchini.

*- Produsa*



**Brian Munene**

Bw rais, usiwahi kusahau kuimarisha "mahasla". Ulitupa ari ya kukupigia kura. Nina hakika utajitahidi kutuinua. Tilia maanani ustawishaji wa uchumi, huduma ya afya na kuunda ajira kwa vijana. Tuna matumaini ya siku za usoni zilizojaa ufanisi. Usituvunje moyo.

*- Dereva*



**Stephanie Mbogua**

Bw rais, "Taifa la Mahasla" lina matumaini makuu. Tunang'ang'ana kujikimu kimaisha kwa kuwa gharama ya maisha imepanda sana. Buni mikakati itakayotoa ajira kwa vijana wengi waliokuunga mkono wakati wa kampeni zako. Hayo ndiyo maombi yangu.

*- Mwanahabari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MTAZAMO WANGU

# SOKO TELEZI LA KUBADILI PESA

**'MKONO MFICHE:** Vikomo katika masuala ya ubadilishaji wa sarafu kidijitali vinapaswa kuwekwa chini ya uangalizi wa serikali. Wafanyabiashara katika soko hili wanapaswa, katika hali za dharura, kuwasilisha historia yao kwa mamlaka.





• NA WAGA ODONGO

Dola ina thamani gani? Kwa sasa ni sarafu isiyo na msimamo. Benki Kuu ya Kenya (CBK) imepania kudumisha dhana kuwa thamani yake ni Sh120.

Benki yangu haiwaamini na inafikiri kuwa dola moja mfukoni mwako ina thamani ndogo tu ya Sh115 lakini itakuuzia sarafu hiyo hiyo kwa bei ghali ya Sh130.

Bei bora ya dola inapatikana katika masoko kadhaa ya hisa kidijitali duniani, ambayo wakati wa kuandika hukuruhusu kununua alama zinazoambatishwa kwenye dola kwa Sh125.4 na kuziuaza alama hizo hizo kwa Sh125.8.

Wakenya wengi, baada ya kuchoshwa na masaibu ya kushuka kwa thamani ya shilingi, wanageukia sarafu thabiti zilizoambatishwa na dola ili kuhifadhi thamani ya kidogo wanachomiliki.

Kwanza, ningependa kukutahadharisha dhidi ya kujihusisha na biashara hii maarufu kama 'crypto'. Inaambatana na hatari nyingi; soko limefurika matapeli na bei nayobadilika ghafla itakuacha umeduwaa. Napendekeza ufuate uraibu unaoweza kutibiwa kwa urahisi zaidi kama unywaji pombe.

Aidha, sitaki kuharibu sifa ya soko la hisa kidijitali; zinawapa ajira vijana wengi Wakenya, baadhi yao wanaojikimu kimaisha kwa kunadi bei ya pesa hizo za kuchekesha kwenye intanenti. Kampuni kama vile Paxful, LocalBitcoins na Binance zinachangia nafasi muhimu sana na ni vigumu kuwaza kwamba zinaweza kupigwa marufuku.

Nataka kufichua sehemu chache dhaifu katika masoko haya zinazoweza kutumiwa vibaya na wahalifu.

Hivi majuzi nilijisajili na shirika moja kuu la biashara ya hisa kidijitali, na karibu dakika kumi baada ya kuwasilisha kitambulisho changu cha kitaifa na sura yangu kupigwa picha, nilipewa kiwango cha kila siku cha kunadi ambacho ni sawa na $8 milioni (karibu Sh960 milioni kwa kutumia kiwango cha dola cha Benki Kuu ya Kenya).

Nchini Kenya, kila wakati unapofanya biashara yenye thamani ya dola 10,000, benki yako inapaswa kutoa ripoti ya shughuli hiyo kwa CBK. M-Pesa inakupa kiwango cha hadi Sh300,000 kwa siku katika vifurushi vya Sh150,000. Hundi inahitajika kuwa chini ya Sh1 million.

Benki moja nchini iliwahi kuniita kwa kutuma Sh550,000 kwa akaunti ambayo sikuwa nimeitumia kwa muda mrefu na kujaribu kutoa pesa hizo sekunde chache baadaye. Pesa hizo zilikuwa chini ya kiwango kisichostahili kupitwa kisheria, ikasema benki, lakini zilitiliwa shaka. Nililazimika kuthibitisha ni zangu kwa kutumia baruameme na nakala za benki.

Hapa tuna jukwaa la biashara ya pesa yenye viwango ambavyo ni maelfu ya kile ambacho benki yako inaweza kutaja kama halali na hata halikuhitaji kutuma nambari ya cheti cha Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru (KRA).

Kinachopaswa kuibua hofu kwa Wakenya na CBK ni mikakati inayowekwa na baadhi ya wauzaji katika masoko haya ili kufanya iwe vigumu kufuatilia biashara hii.

Muuzaji mmoja kwenye mtandao huo aliye na zaidi ya dola milioni moja, anasema katika tawasifu yake kwamba, kwa bei ya thamani ya zaidi ya Sh350,000 malipo kupitia benki yatagawanywa katika vitengo vidogo vidogo, visivyoweza kuonekana. Hatachukua ombi la kiwango cha chini ya Sh100,000.

Mfanyabiashara mwingine anafafanua kuwa unaweza kumtupa nje wakala – akaunti sumbufu za M-Pesa na benki – na kubadilisha sarafu tasilimu kwa thamani za dola, hayo yote kwa ada nafuu ya asilimia tatu. Hii inaondoa ushahidi wowote wa mkondo wa kidijitali.

Karibu mwongo mmoja uliopita, akaunti ya benki ya Anthony Chinedu, raia wa Nigeria aliyezua sarakasi kati yake na mwanamke Mkenya, Akinyi, ilifungwa alipojaribu kuweka mamilioni ya pesa. Baadaye alirudishwa kwao kwa madai ya ulanguzi wa mihadarati.

Leo hii, mtu anayehitaji kwa dharura kubadilisha pesa katika sarafu inayokubalika kwa urahisi kidijitali hawezi kwenda benki bali kwenye mtandao wa kubadilisha sarafu kidijitali.

Baada ya shambulizi la Westgate, makachero waligundua mtandao uliohusika kwa kuchunguza shughuli za benki za gaidi mmoja. Kwa taifa linalokabiliwa na mashambulizi ya kigaidi mara kwa mara, ni muhimu kuwa baada ya shambulizi, wapelelezi wanaweza kujua haraka historia ya kifedha ya mshukiwa ili kuwapata washukiwa wengine. Ugaidi unaegemea zaidi vijana na wanaume, kundi ambalo historia yake ya kifedha siku hizi aghalabu inajumuisha fedha kidijitali.

Biashara hii ya kubadili fedha si mpya. Imekuwapo kwa mwongo mmoja. Kilicho tofauti ni kiwango chake na vitengo tele vinavyoshughulikia soko la sasa.

Biashara ya crypto sasa ni mifumo thabiti ambayo watumiaji wake hawahitaji kamwe kuondoka na ambayo maafisa wetu wa CBK huenda wasiweze kuchungulia kuona shughuli zao.

Haijabainika wazi iwapo wahusika hutoa maelezo ya biashara kwa CBK au la. Nitakisia huwa hawafanyi hivyo. Usiri huvaliwa kama gauni la heshima katika biashara ya crypto; hakika jina "crypto" lenyewe linamaanisha fiche.

Maoni yangu ni kuwa viwango katika biashara hii vinapaswa kudhibitiwa na serikali. Wafanyabishara katika mitandao hii wanapaswa, ikiwa kuna dharura, kuwasilisha historia yao kwa mamlaka.

Kiwango cha hadi Shilingi bilioni moja ni mzaha na fedha kama hizo zinapaswa tu kutolewa kwa taasisi husika. Wakati huo vile vile, matangazo ya kubadili sarafu kidijitali yanapaswa kuruhusiwa viwango vya chini pekee.

*Bw Odongo ni mchanganuzi wa crypto.*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media




**Brad Osumo (kulia), mmiliki wa mkahawa wa The Big Fish, mtaa wa Westlands, akiwa kazini Septemba 15.** PICHA | EVANS HABIL

LISHE KWA TAIFA

# SAMAKI ANAYENASA WATU

**NAMNA YA KUSHIBISHA WATU:** Osumo Brad anaonekana kupata mbinu ya kuvutia wateja wa hadhi ya juu kwa biashara yake ya mkahawa unaokuwa kwa kasi.

• NA EDDY ASHIOYA

Ni mtu wa shughuli nyingi. Hiyo ni kutokana na ninayoshuhudia katika mkahawa wake ambao ulipata umaarufu kupitia mtandao wa Twitter, ikizingatiwa mimi ni mwandishi chipukizi.

Sawa na Masia katika Bibilia Takatifu, sasa analisha maelfu ya watu ambao wanafahamu mkahawa huo kupitia mtandao wa Twitter.

Anachuma pato lake kwa kuuza samaki. Si mwingine ila ni Osumo Brad, mfanyabiashara wa samaki mwenye umri wa miaka 29, akifanya kazi aliyopewa na Mungu – kufungua mkahawa wa "The Big Fish Restaurant" ambako watu wa matabaka mbalimbali hukutana siku za Ijumaa, siku ambayo kila mtu huwa tayari kukaribisha wikendi kama Mungu alivyopanga - kwa tumbo lililoshiba samaki.

Inaonekana Nairobi ina mikahawa kadhaa ya kuuza samaki kwa sababu kitoweo hicho kinapendwa sana. Kuna K'Osewes, Mama Oliech na sasa The Big Fish. Kwa nini akafungua The Big Fish? "Nilitaka kila mtu ajue hapa kama mahali unaweza kupata samaki mzuri. Tulitaka kujulikana na kuwa maarufu." Anaonekana kuwa mtu anayependa ukweli na anayeweza kutegemewa.

Hivi majuzi The Big Fish ulitembelewa na wanasiasa wa haiba kubwa akiwemo aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga na kiongozi wa Narc Kenya Martha Karua. Wakili na mwanasiasa Nelson Havi pia amewahi kula hapo.

Tangu hapo kila mtu anataka kuonja kile ambacho Baba (Raila) alikula katika mkahawa huo. Je, mwenye mkahawa huo anaweza kuhudumia wateja wengi? "Nadhani ninaweza. Tumeajiri wafanyakazi karibu 40."

Naungama kuwa sipendi mlo wa samaki, lakini ninaweza kushawishiwa kula. Mbona akaamua kuuza samaki?

"Nililelewa katika Kaunti ya Migori. Niliku-ja Nairobi kutafuta kazi, lakini sikufaulu. Niliamua kujaribu bahati kwingine nione kama ningefaulu. Sasa tunawapikia samaki wateja wetu jinsi tunavyopika samaki nyumbani."

Kazi aliyokuwa akitafuta inahusu taaluma ya kemia aliyosomea katika chuo kikuu. Alikosa kazi na badala ya kukaa nyumbani kulalamika kupitia mtandao wa twitter, akaamua kushirikiana na dada yake, ambaye alikuwa akiuza samaki kando mwa barabara. Ushirika wao ulikuwa wa nipe-nikupe.

Dada yake akitayarisha vyakula, Brad alishughulikia wateja. Ni kupitia Twitter ambapo walipata msukumo wa kutimiza ndoto yao.

Kwa haraka, mmojawapo wa mikahawa

**29** Umri Osuna Brad, ambaye mwenye mikahawa miwili maarufu jijini Nairobi. Kuanzia tawi la kwanza katika eneo la Roasters, mtaa wa Garden Estate, lililofunguliwa miaka mine iliyopita, juzi alifungua tawi lingine katika barabara ya Church Road, mtaa wa Westlands.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

**Kwa haraka, mmoja wa mikahawa maarufu jijini Nairobi unaouza samaki pia uligeuka kuwa ubora zaidi. Kuanzia tawi la kwanza katika Roasters, mtaa wa Garden, lililofunguliwa miaka minne iliyopita, juzi walifungua tawi lingine katika barabara ya Church Road, mtaani Westlands.**

maarufu jijini Nairobi unaouza samaki pia uligeuka kuwa wenye ubora zaidi.Kuanzia tawi lao la kwanza katika eneo Roasters, mtaa wa Garden, lililofunguliwa miaka minne iliyopita, juzi walifungua tawi lingine katika barabara ya Church Road, mtaani Westlands.

Je, mambo yameendea alivyotarajia? "Sikuwa na matumaini makubwa. Nilitamani tu kuwa gari na nyumba. Lakini Big Fish imenifikisha mbali."

Nafikiria kuhusu mzaha ambao natamani sana kufanya naye. "Ningefungua biashara hii pamoja na watu wengine lakini kila mara mwalimu wangu alinishauri kulenga juu - kulenga Samaki Mkubwa."

Hanielewi kwa hivyo ninaendelea. Yeye hutumia pesa zake vipi? "Unajua, mimi sinywi pombe, lakini ninatumia wakati wangu mwingi katika vilabu vya burudani. Hata sijinunulii chochote, unajua?"

Amezoea kukamilisha kila semi zake kwa kusema "unajua".

Nimejua, kutokana na changamoto zake, kwamba ni Afisa Mkuu Mtendaji wa kipekee. Anaongoza kwa moyo. Ni meneja asiyevalia jezi na long'i chapa 'jeans'.

"Wakati huu ninapokea idadi kubwa ya watu wakitaka ushauri na mwelekeo kutoka kwangu. Ukiwa na biashara wewe ni kama mzazi. Watu wote wanatarajia kuwa unaelewa vyema mambo mengi kuhusu maisha. Huo ni mzigo ambao utabeba, wajua?"

"Ufanisi ni kufanya unachofurahia. Si pesa tu, ni kuridhika moyoni. Kuna watu wanaoanza kitu kisha wanaacha, lakini ukiwa na bidii na mvumilivu katika unachoyafanya, bila shaka utafaulu na kufurahia, wajua?"

Hata hivyo, anakumbuka kuwa alifeli wakati fulani katika shughuli zake za biashara kiasi kwamba alilazimika kujiondoa kwa muda.

Mnamo 2018, biashara ilikuwa mbaya na akalazimika kuyoyomea vijijini akiapa kutogusa samaki tena. Lakini alibadili nia na kuamua kurejeleaudia biashara hiyo na sasa anavuna matunda ya uvumilivu huo.

Ninapata fursa na kumuuliza swali ambalo nimekuwa nikitamani kumuuliza: Je, ni heri kuwa samaki mdogo ndani ya kidimbwi kikubwa ama samaki mkubwa ndani ya kidimbwi kidogo?

"Heri niwe samaki mdogo ndani ya kidimbwi kikubwa. Unapata changamoto zaidi na ukizishinda unaona fahari. Unakabili maisha ukijihisi mnyonge lakini baadaye, unafaulu, wajua?" Najua.

## Heri niwe samaki mdogo ndani ya kidimbwi kikubwa. Unapata changamoto zaidi na ukizishinda unaona fahari. Unakabili maisha ukiamini akilini mwako kuwa wewe ni mnyonge lakini baadaye, unafaulu, wajua?

Osumo Brad



Mkahawa wa The Big Fish, Mtaa wa Westlands, Nairobi, mnamo Septemba 15. PICHA | EVANS HABIL

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MBIO ZA MIUNGU

# BINGWA CHIPUKIZI WA KASI

**USTADI WA KUTISHA:** Dereva wa ajabu, McRae Kimathi amezuzua halaiki kote ulimwenguni. Anataka kuwa dereva wa kwanza kutoka Afrika Mashariki kushiriki mbio za magari kama taaluma na, ikiwezekana, avutie wengine miaka ijayo




**McRae Kimathi alikuwa dereva pekee Mwafrika asili miongoni mwa madereva Wanane wa Kwanza kumaliza mbio za magari za Equator Rally mjini Naivasha mnamo 2021. CHINI: Akishirikiana na dereva-mwenza Mwangi Kioni, Kimathi atifua vumbi na gari lake aina ya Ford Fiesta wakati wa mbio za Equator Rally mnamo April 1, 2022.** PICHA I ANWAR SIDI NA SILAS KIPLAGAT

• NA PETER NJENGA

Karibu McRae Kimathi aguse miungu wa zama wa Ugiriki wikendi iliyopita, kwa kudhihirisha taaluma yake inayoendelea kukua iliyoanzia Kenya lakini ikavuma Ulaya kama upepo mkali na kushtua kijiji kitulivu barani Asia.

Akishirikiana na Mwangi Kioni, dereva huyo mchanga wa mbio za magari anabomoa mtazamo kwamba Mwafrika mweusi hawezi kubobea katika mashindano ya mbio za magari. Anafuata ndoto ya dereva aliyemvutia tangu akiwa tineja, bingwa mara saba wa dunia wa mashindano ya Formula One, Lewis Hamilton, ambaye alizuru Kenya majuzi.




Hamilton amedhihirisha kuwa mtu mweusi ana uwezo mkubwa katika mambo mengi hasa masuala ya kasi.

Kimathi, 27, alikamilisha ratiba kali ya mbio za magari iliyompeleka kwenye theluji na baridi ya msimu wa baridi wa nchi za Scandinavia, Sweden, Croatia na Estonia, kabla ya kushiriki mbio hizo nchi yenye mawe ya Ureno na hatimaye kuingia kwa ushindi Ugiriki, nchi inayosifiwa kama nyumbani kwa wasanifu mijengo, wanafilosofia, wanahisibati na michezo.

Kimathi alimaliza mbio za magari za ulimwengu za EPO Acropolis International Automobile Federation (FIA) World Rally Championship, Acropolis Rally, zilizofanywa katika milima ya Kamena Vourla, kilomita 250 kutoka jiji kuu Jumapili iliyopita. Sasa anajiandaa kwa msimu wenye shughuli nyingi kimataifa katika juhudi zake za kuwa dereva wa kwanza kutoka Afrika Mashariki kushiriki mbio za magari kama taaluma na kutarajia kuwa shughuli zake zitavutia vizazi vya miaka ijayo.

Mashindano ya mbio za magari ya Acropolis Rally yanajulikana kama "Mbio za Miungu". Kama aliwagusa au la, hiyo sasa ni hadithi. Hata hivyo, Kimathi alipata hisia za ndani za kujiamini. "Nilianza msimu Uswizi kama mvulana. Leo najihisi kuwa tineja, na

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



McRae Kimathi na dereva-mwenza Mwangi Kioni kabla ya kuanza mbio za WRC Safari Rally katika Uwanja wa Kimataifa wa Moi, Kasarani, mnamo Juni 17. PICHA | SILAS KIPLAGAT

kutoka hapa, ninaweza kuwa tu mwanamume katika mbio za magari. Umekuwa msimu mrefu, mgumu sana. Nafurahia matokeo yake," alisema Kimathi akiwa Ugiriki.

"Mtu huendelea kujifunza. Kushiriki kwa wakati mmoja mashindano ya Afrika na ya ulimwengu kumekuwa changamoto. Nafikiri huu ni msimu ambao nimeshiriki mbio nyingi zaidi katika maisha yangu. Nimejifunza mengi. Kasi yangu imeimarika."

Mwembamba, mrefu na asiye na kiburi, mwanafunzi huyu wa zamani wa Chuo Kikuu cha Strathmore ana nidhamu.

Kimathi alimaliza msimu wa 2022 wa mashindano ya Junior World Rally Championship katika nafasi ya tano baada ya mbio za Uswizi, Croatia, Ureno, Estonia na Ugiriki.

Alianza mbio hizo katika mashindano ya mbio za kitaifa za magari Kenya mwaka wa 2015 zilizofanywa Naivasha na ingawa alikuwa miongoni mwa kumi bora, alipata ubatizo wa moto.

Alibadilisha mawazo yake tangu wakati huo. Mbio za magari ni hafla ya mchezo unaohitaji nidhamu na hali nzuri ya mwili na akili. Alizaliwa na kulelewa katika mazingira ya mbio za magari, akipata msukumo kutoka kwa baba yake, Phineas Kimathi, mtu wa kwanza kupatia kampuni ya magari ya Hyundai Motor Corporation alama za kwanza katika mbio za magari ulimwenguni kwa kushinda kitengo cha F2 katika mashindano ya Safari Rally mwaka wa 1999.

"Nasubiri msimu ujao. Wamejitolea sana katika uendeshaji wao wa magari. Nina hakika ninaweza kwenda mbali nikipata mafunzo na uzoefu," anasema Kimathi mdogo.

Akiwa kifungua mimba katika familia ya watoto watatu, Kimathi amekuwa akishiriki mbio za magari chini ya timu ya wataalamu wa mbio hizo, M-Sport Poland, ambayo imewekeza sana katika kazi yake, ikiwemo kumpa mafunzo kuhusu uendeshaji gari kwenye theluji huko Gelio, Norway.

" Nilianza kushiriki mbio za magari 2015. Nilishiriki mbio kadhaa nje na hapa nchini. Kisha nikagundua nilihitaji kitu cha maana kunifanya kuwa dereva bora," akasema.

"Nikiwa na hili akilini, nilishiriki shindano la Autocross mwaka wa 2017 na kuibuka wa pili. Mwaka wa 2018, nilikuwa wa tatu." Pia aligundua kwamba pupa si sifa njema kamwe.

"Nikiwa na umri wa miaka 17 na mwenye ari, baba yangu alikuwa na gari aina ya Subaru Forester na siku za Jumapili nilikuwa nikitoka nalo. Jumapili moja, niliendesha kwa kasi, nikagonga kikingi cha stima na likabingiria. Ilikuwa ajali mbaya lakini nashukuru Mungu sikujeruhiwa."

Tukio hilo lilimfunza umuhimu wa kuheshimu magari na kupata mafunzo ili kuwa dereva wa mbio za magari.

Je, lilikuwa funzo lenye thamani kwake? "Ajali hiyo ilinifunza mambo mengi. Kwanza, niligundua uwezo wangu na hatari za mchezo wa kuendesha magari," akasema. "Pia, ilitekeleza sehemu kisaikolojia katika siku za mwanzo za kazi yangu ya mashindano ya mbio za magari, kwa kuwa nilikuwa na hofu kiasi.

"Katika mashindano ya mbio za magari, lazima uwe mtu mwenye nguvu. Niliisahau haraka na kusonga mbele. Ilinifanya kuwajibika zaidi nje ya mchezo."

Na kwa hakika, tabia yake tulivu imemfanya kuwa dereva wa mbio za magari mwenye matumaini makubwa Afrika, nafasi ya kumezewa mate inayoendelea kuhimiza madereva wengine Kenya.

## 1999

Phineas Kimathi, mtu wa kwanza kupatia kampuni ya magari ya Hyundai Motor Corporation alama za kwanza katika mbio za magari ulimwenguni kwa kushinda kitengo cha F2 katika mashindano ya Safari Rally.

## UONGOZI MPYA

*Na J. Nyaganyagah*

jnyaga@ke.nationmedia.com




## NYOTA WA WIKI

MOJAWAPO LA KISA CHA KUTIA MOYO KUTOKANA NA UCHAGUZI MKUU ULIOKAMILIKA MAJUZI NI KILE CHA MBUNGE WA MUMIAS EAST, PETER SALASYA, MWENYE UMRI WA MIAKA 30.

SAFARI YAKE YA KISIASA IMEKUWA NA CHANGAMOTO NYINGI SANA. ALIANZA KWA KUSHINDWA VIBAYA KATIKA CHUO KIKUU CHA EGERTON ALIPOGOMBEA KITI CHA MKURUGENZI WA MASOMO AKIWA KIDATO CHA KWANZA.

JARIBIO LAKE LA KWANZA LA KUWA MBUNGE LILIZIMWA KWA KUSHINDWA TENA VIBAYA NA KUIBUKA WA MWISHO KWA KURA 254 PEKEE KATIKA UCHAGUZI MKUU WA 2017. BAADAYE ALIPOTEZA KAZI YAKE KATIKA BENKI NA KUAJIRIWA KIBARUA CHA KUFUNZA ILI KUJIKIMU KIMAISHA HUKU AKISHIKILIA NDOTO YAKE.



JUHUDI ZAKE HATIMAYE ZILIZAA MATUNDA ALIPOSHINDA KITI CHA BUNGE CHA MUMIAS BILA PESA ZOZOTE MFUKONI, NA KUWABWAGA WANASIASA WAKONGWE NA WENYE PESA. MAKOFI KWA MHESHIMIWA SALASYA.

Nation Media Group "ePaper Copy"

tahariri




■ Saidia na kuwekeza katika biashara ndogo ndogo na sekta ya jua kali.

# Mfumo wa 'Bottom-up' unafaa kutuinua

Je, inawezekana msemo kuwa 'ni mazuri yote yanayoisha vizuri' ulitimia Jumanne? Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta alipokuwa akimkabidhi mamlaka Rais mpya William Ruto, mjadala ulianza kuhusu maana halisi ya wakati huo kwa wawili hao na Kenya kwa jumla. Ulikuwa wakati mchungu kwa Rais Kenyatta na mchungu - mtamu kwa Dkt Ruto.

Sifa ya kisiasa ya viongozi hao wawili itakumbukwa kwa jinsi tofauti sana, hasa ikizingatiwa Rais Kenyatta alimkabidhi mamlaka kiongozi ambaye hakutaka awe mrithi wake. Vile vile, hakumpa pongezi hata baada ya kushinda urais.

Wawili hao walishinda urais 2013 na mara mbili 2017. Mnamo 2012, walishtakiwa pamoja katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kwa uhalifu wa kibinadamu.

Licha ya kukabiliwa na mashtaka hayo mazito, bado waliibuka washindi kutokana na shutuma za hapa nchini dhidi ya kuhusu mahakama hiyo ya kigeni. Wengi walichukulia hatua hiyo kuwa wageni kuingilia nchi yao.

Waligawana serikali asilimia hamsini kila mmoja. Walivalia mavazi yaliyofanana; kama ndugu wa mama mmoja. Walisalimiana na kuonyesha urafiki ambao haukuwa umeshuhudiwa awali katika ulingo wa kisiasa nchini.

Kutokana na urafiki huo, Wakenya wengi walidhani wamechagua marais wawili kwa pamoja.

**Shughuli ya mpito iliendelea vyema mbele ya marais 20 na umati uliojawa na furaha katika Uwanja wa Michezo wa Moi, Kasarani. Baada ya miaka minne ya makabiliano makali ya kisiasa, ulikuwa wakati wa kugeukia shughuli nyingine za kujenga nchi.**



KWENDO OPANGA

Lakini mwezi uliopita, Bw Kenyatta alitangaza wazi kuwa, ingawa Katiba inamtaka kumkabidhi mamlaka mshindi baada ya uchaguzi, alimpendelea Bw Raila Odinga kuwa mrithi wake. Bw Kenyatta pia alimfanyia kampeni Bw Odinga lakini hakufanikiwa kushinda urais.

Shughuli ya kukabidhi mamlaka iliendelea vyema mbele ya marais 20 na umati uliojawa na furaha katika Uwanja wa Michezo wa Kasarani, Nairobi. Baada ya miaka minne ya makabiliano makali ya kisiasa, ulikuwa wakati wa kugeukia shughuli nyingine za kujenga nchi.

Shughuli za ujenzi wa taifa lazima ziongozwe na Rais Ruto, aliyekita sera zake za kiuchumi katika kuwainua watu wa kiwango cha chini.

Siasa za 'Mahasla' (watu wanyonge) zinajenga imani kwa watoto wa wananchi maskini kuwa wanaweza kupaa na kutwaa nafasi za juu za uongozi kama Dkt Ruto, ambaye amehudumu kama naibu waziri, waziri, Naibu Rais na sasa Rais.

Kuna nguzo mbili kuu za mfumo wa kiuchumi wa kuinua maskini. Moja, ni jukumu la serikali kubuni nafasi za ajira kwa vijana ili kuwawezesha kushiriki kwenye ujenzi wa taifa kwa kubuni utajiri, kupata ajira na kuendesha biashara. Hapa pia, watoto wa maskini wako na nafasi ya kupiga hatua kama Dkt Ruto. Wakipewa nafasi inayofaa, wanaweza kujijenga kwa kuanzisha biashara ndogo ndogo, na baadaye kuzipanua hadi viwango vya kimataifa. Ni hali inayoweza kuchangia sana ukuaji wa uchumi wa nchi.

Nguzo ya pili inaeleza kuwa tangu uhuru, Kenya imekuwa ikiendesha sera za kiuchumi ambazo zimekuwa zikishinikiza ukuaji wa kampuni na mashirika makubwa ya kibiashara. Ni mfumo unaolaumiwa kwa kutoboresha maisha ya Wakenya wengi. Nguzo hii inaeleza kuwa Wakenya wengi - zaidi ya asilimia 70 - wameajiriwa ama kujiajiri katika biashara ndogo ndogo au za kadri.

Hivyo, ni wakati wa serikali kuanza kuinua biashara hizo kwa kuwasaidia wafanyabiashara kuzipanua.

Kwa jumla, sera ya kiuchumi ya kuwainua maskini na siasa za 'mahasla' zinaonyesha dalili za kuboresha umoja na utangamano nchini. Kwenye kampeni zao, vigogo wakuu wa mrengo wa Kenya Kwanza walipigia debe sera hizo, wakishikilia kwamba hakuna mtu ama eneo litakalotengwa kwenye harakati za kustawisha nchi kiuchumi.

Akiwa juu, lazima Rais Ruto aongoze kutoka chini.

*kwendo58@gmail.com*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

■ Tunahitaji kutafuta namna ya kuepuka hasira na migawanyiko wakati wa uchaguzi

# Uchaguzi umeisha, sasa tuponye taifa



MACHARIA GAITHO

"Kubali na uendelee na maisha yako." Hiyo ndiyo kauli ya washindi wa chaguzi, iwe ni kwa njia halali ama haramu, kwa wanaoshindwa na kupinga matokeo.

Huu ni ujumbe ambao ni tunafaa kusisitiza, ikizingatiwa kuwa uchaguzi umeisha na ni lazima tukubali ukweli wa mambo Ikulu imepata mpangaji mpya. Kubali na uendelee na maisha.

La, sizungumzii mgombea urais aliyeshindwa, Bw Raila Odinga na mgombea-mwenza, Bi Martha Karua wala wafuasi wao mamilioni; bali Rais William Ruto na Naibu Rais Rigathi Gachagua, ambao waliapishwa Jumanne iliyopita wakionekana kuwa na maruerue ya kampeni.

Uchaguzi umeisha, Bw Rais na Bw Gachagua, na sasa mtakuwa uongozini kwa miaka mitano ijayo. Kubalini na msonge mbele. Hiakuwa picha nzuri hata kidogo. Hafla ya kitaifa iliyohudhuriwa na wageni maarufu kutoka sehemu tofauti duniani, wakiwemo marais 20, iligeuzwa kuwa jukwaa la matusi na lawama kama ilivyokuwa kwenye mikutano ya kampeni.

Ikizingatiwa kuwa hafla hiyo ilikuwa ikipeperushwa moja kwa moja katika sehemu tofauti duniani, ilipaswa kuwa nafasi ya kuonyesha mfano bora wa demokrasia komavu inayopaswa kuigwa na Afrika na mataifa ambayo bado yanakua kidemokrasia.


Viongozi waliokuwepo walifaa kuona mfumo uliokomaa wa utawala, ambapo mamlaka hupitishwa kutoka kwa rais mmoja hadi mwingine katika hali tulivu na yafuraha.

Badala yake, marais Yoweri Museveni (Uganda), Evariste Ndayishime (Burundi), Umaro Mokhtar Sissoco Embalo (Guinea Bissau), Paul Kamage (Rwanda) miongoni mwa wengine waliotawala nchi zao kwa miaka mingi, walipata sababu, imani na hakikisho la kuendelea kukatalia mamlakani. Hafla hiyo ilitawaliwa na hasira na machungu makubwa.

Tuliyoshuhudia yanaonyesha kuwa kuna haja ya kuanzishwa mafunzo ya kudhibiti hasira katika Ikulu na Makao Rasmi ya Naibu Rais.

Wakati huo huo, tunapoanza utawala mpya kwa matumaini, ni lazima tutathmini athari

**Hafla hiyo ilipeperushwa moja kwa moja sehemu tofauti duniani na ilipaswa kuwa nafasi ya kuonyesha mfano bora wa demokrasia komavu inayofaa kuigwa na Afrika na mataifa yanayokua kidemokrasia. Viongozi waliokuwepo walifaa kuona mfumo uliokomaa wa utawala, ambapo mamlaka hupitishwa kutoka kwa rais mmoja hadi mwingine katika hali tulivu na yafuraha.**



Naibu Rais Rigathi Gachagua akiapishwa huku mkewe, Dorcas Gachagua, akitazama katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Moi, Kasarani, Septemba 13. Kiapo hicho kiliongozwa na Msajili Mkuu wa Mahakama, Anne Amadi (kushoto), na kushuhudiwa na Jaji Mkuu na Rais wa Mahakama ya Upeo, Martha Koome. PICHA | SILA KIPLAGAT

za wanaotuongoza, kuhusu iwapo wataongoza nchi wakiwa wamejawa na hasira.

Kuna mtindo wa viongozi wa aina hiyo kutoangalia mbele na badala yake kuendelea kuwalaumu wapinzani au watangulizi wao kwa makosa yao wenyewe. Wanaweza hata kulipiza kisasi dhidi ya watu wanaowachukia.

Hotuba ya Rais Ruto ilikuwa nzuri, kwani iliangazia ajenda aliyo nayo na changamoto nyingi alizopitia. Vile vile, alichukua muda kutambua na kuwapongeza washindani wake.

Hata hivyo, alikumbwa na matatizo mara kadhaa katika hotuba yake iliyoandikwa, na kumfanya kutoa kauli chache ambazo hazikuwa katika hotuba hiyo. Alionekana kumuiga Bw Gachagua, aliyetumia nafasi hiyo kutoa kauli ambazo kamwe hakufaa kuzitoa wala kuzitaja katika hafla hiyo muhimu.

Lawama na ukosoaji wa Bw Gachagua dhidi ya Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta kamwe hazikufaa. Zilimuonyesha kuwa mtu mwenye kisasi, asiyeweza kuaminika kushikilia nafasi kubwa ya uongozi. Hotuba yake ilikuwa ya kutia hofu kutokana na vitisho alivyotoa. Ni hotuba iliyotufanya kuwa na wasiwasi mkubwa.

Hata hivyo, alitukumbusha kuwa vitendo vyetu sisi wenyewe ndivyo vinafaa kuhakikisha kuwa demokrasia inalindwa na kuendelea nchini.

Katika suala lilo hilo, lazima tuwahimize Bw Odinga na Bi Karua kukubali matokeo ya uchaguzi na kuchukua mtazamo mpya. Halikuwa jambo zuri kwao kususia hafla hiyo hata kama hawakubaliani na uamuzi wa Korti ya Upeo.

Bi Karua ameeleza kwamba ataelekeza malalamishi yake kuhusu uchaguzi huo katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki, jijini Arusha, Tanzania. Hiyo ni haki yake, ingawa sijui kama nitacheka ama nitalia. Mimi si msomi wa sheria kama mawakili, lakini, kulingana na ufahamu wangu mdogo wa masuala ya haki, hatua hiyo haitazaa matunda yoyote.

Bw Odinga na Bi Karua wana mengi muhimu wanayoweza kufanya badala ya kuendelea kulalamika kuhusu matokeo ya uchaguzi uliokamilika. Kwanza, wanaweza kuagiza uchunguzi huru kuhusu tatizo lililoibuka kwenye kampeni za mrengo wa Azimio. Kuna uwezekano kuwa tatizo kuu lililoibuka ni muungano huo kujiamini sana kwa kuungwa mkono na serikali.

Vile vile, wanaweza kuchunguza ni kwa nini ushahidi waliowasilisha katika Mahakama ya Upeo haukutosha, hasa hatua yao kushindwa kuthibitisha tofauti za matokeo kwenye Fomu 34A walizowasilisha mahakamani. La muhimu zaidi ni kuwa wana ufuasi katika karibu nusu ya nchi nzima. Hilo ni eneo na idadi kubwa ya watu wanaohitaji uongozi.

Upinzani wenye nguvu bado unahitajika ili kulinda vitisho na ukiukaji wowote wa demokrasia, haki za binadamu, uhuru wa kujieleza na kurejea kwa utawala wa kiimla na uporaji wa mali ya umma, kama ilivyokuwa nyakati za Moi. Kama hali nchini ni ile tuliyoshuhudia wakati wa kuapishwa kwa

Rais Ruto, basi juhudi na mikakati ya kuleta utangamano zinahitajika kwa dharura.

Lazima mdahalo wa kitaifa uwepo kuhusu matatizo yanayokumba uchaguzi wetu na migawanyiko inayotokea baadaye. Lazima pia tutathmini kutofaulu kwa juhudi za awali za kuleta usawa wa kijamii. Ilitarajiwa Mpango wa Kubadilisha Katiba (BBI) ungefeli, baada ya kuingizwa siasa, badala ya kukitwa kwenye juhudi za kuleta umoja wa kitaifa.

Kuna nafasi ya uongozi kuhusu masuala hayo. Wadau wa kisiasa watakaoungana na mashirika ya kutetea haki za umma, vyama vya wanataaluma, makundi ya kidini, vyama vya

Wafanyakazi na makundi ya kijamii wanaweza kubuni miungano yenye nguvu itakayobuni mwongozo kuhusu jinsi ya kujenga Kenya tunayotaka.

*gaithomail@gmail.com*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

USHINDANI WA MAMLAKA MAGHARIBI MWA KENYA

# UBABE WA NDUGU WANUKIA

*Tayari, ndugu wa kisiasa, Mudavadi na Wetang'ula, kila mmoja anaamini ndiye 'wa tatu' kwa uwezo wa kisiasa na mamlaka ya uongozi baada ya Rais Ruto na Naibu Rais Gachagua*



Musalia Mudavadi

• Na OSCAR OBONYO

Katika mojawapo ya njama za siri zaidi kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu, washauri wa Rais Uhuru Kenyatta walimtambua Kiongozi wa chama cha Amani National Congress (ANC) Musalia Mudavadi kuwa waliyependelea awe mrithi wake. Hata hivyo, katikati ya utekelezaji wa mpango wao 2019, waligeuza macho kwa kiongozi wa chama cha Orange Democratic Movement (ODM), Raila Odinga, kwa sababu waliona kama aliyeweza kuwakilisha maslahi yao vyema.

Bw David Murathe, mshirika wa karibu sana wa Rais mstaafu Uhuru Kenyatta na mmoja wa waliokuwa wakipanga mikakati ya mpito, anaeleza kwamba uamuzi wa mwanzo wa kutambua kiongozi huyo wa chama cha ANC kuwa mrithi wa urais, ulitokana na uzoefu wake wa kisiasa na mwonekano wake kitaifa.

Mudavadi pia alichukuliwa kuwa kiongozi aliye ushirikiano wa kisiasa na uhusiano wa muda mrefu na Bw Kenyatta. Katika utathmini wao, hata hivyo, mwonekano wa Musalia kama "mtu mzuri" na kuwa mwanasiasa muungwana hazikutosha kutimiza lengo lao kuu, ambalo lilikuwa ni kumzuia Naibu wa Bw Kenyatta, Dkt William Samoei Ruto kushinda urais.

Juhudi za nyuma ya pazia zilimchagua Bw Odinga, mwanasiasa mzoefu wa miaka mingi aliyekuwa amegombea urais mara nne, ambaye Murathe anasema "alikuwa na ufuasi mkubwa mashinani na wa pekee kuweza kumzima William".

Kwa hivyo kwa kutegemea yaliyopita, huenda Murathe alisema kweli kumhusu Musalia, aliposema "hakuwa na uwezo wa kumzima Ruto". Hiyo ni kwa sababu hasa alifaulu kufanya kinyume - kusaidia Ruto kushinda urais.

Akishirikiana na mwenzake wa Ford-Kenya, Moses Wetang'ula, ambaye alichaguliwa Spika wa Bunge la Kitaifa siku chache zilizopita, Musalia anafurahia kukataa ombi la Bw Kenyatta amuunge mkono Odinga kwa urais. Katika hatua kubwa iliyojaa vituko ya kukataa ombi hilo inayofahamika kama "Tetemeko la Ardhi", Musalia alimuunga mkono Ruto na leo anatazama siku zake za baadaye kisiasa na zile za ngome yake ya magharibi ya Kenya kwa matumaini.

Kwa Wetang'ula kuchaguliwa Spika wa Bunge la Taifa naye kuteuliwa Mkuu wa Mawaziri, msisimko na furaha miongoni mwa wapiga kura katika eneo la magharibi mwa Kenya inaeleweka.

Ingawa wawili hao walimpa Ruto kura chache za rais katika eneo hilo zikilinganishwa na za Raila na kushinda viti vichache vya kuchaguliwa vya ugavana na ubunge, ushindi wa Ruto ni hatua muhimu kwao. Hatua hiyo imewawezesha kushikilia nyadhifa kuu za kitaifa na kuwapa fursa ya kugeuza eneo hilo upande wao.

Katika hali iliyopo makabiliano ya kisiasa na Odinga hayaepukiki. Akiwa naibu kiongozi wa chama cha ODM, aliyekuwa Gavana wa Kakamega, Wycliffe Ambetsa Oparanya, ni nguzo ya wafuasi wa Bw Odinga katika eneo hilo na atapambana vikali kulinda alichopigania kwa bidii kukipata.

Mbali na kushinda viti 10 kati ya 12 vya ubunge Kaunti ya Kakamega, Oparanya, ambaye aliongoza kampeni za Azimio katika eneo hilo, pia alipata ushindi mkubwa katika Kaunti ya Busia, na nyumbani kwa Mudavadi, Vihiga, ambako Azimio ilishinda viti vya Gavana na Seneta. Kuendelea mbele, huu ndio ufanisi ambao Musalia na Wetang'ula watapambana kutwaa kutoka kwa Oparanya, na kwa kufanya hivyo Raila, jambo ambalo litazua vita vya kufurahisha vya kisiasa katika siku zijazo.

Lakini, pengine vita vibaya zaidi, na ambavyo hakuna anayevizungumzia,

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

huenda vikatoka ndani - kati ya kaka wawili, Musalia na Wetang'ula. Dkt Henry Wabwire, mchanganuzi wa siasa, anasema Musalia na Wetang'ula hawawezi kuwa wasemaji wa Ruto katika eneo hili kwa wakati mmoja na pia kuwa viongozi wa jamii ya Waluhya pamoja, au hata kuungana kugombea urais katika uchaguzi ujao.

"Kwa kujiweka katika hatari ya kuonekana kuzua mgawanyiko kati ya kaka hao wawili wa kisiasa, lazima niseme wazi kuwa wawili hao watapigana kila mmoja akisaka ushawishi wa kisiasa na kujiandaa kabla ya uchaguzi mkuu ujao. Ni hali ya siasa," anasema Dkt Wabwire.

Tayari, Wetang'ula na Musalia kila mmoja anaamini ndiye "wa tatu mkuu kwa mamlaka" ya kisiasa baada ya Rais William Ruto na Naibu Rais Rigathi Gachagua. Kwa hakika, ushindani wa ndani wa kisiasa ni uovu mmoja ambao viongozi hao wawili watajitahidi kuondoa ili kuepuka kile ambacho watangulizi wao katika siasa walishindwa kufanya.

Tofauti na jamii jirani ya Waluo, Wakikuyu na Wakalenjin, ambao wanaunga mkono kiongozi wao mmoja kila wakati, hali ya Waluhya kwa miaka mingi imekuwa ya uhasama mkubwa wa kisiasa huku jamii hiyo ikigawanyika. Kwa mfano, Rais Daniel arap Moi wa chama tawala cha Kanu alipomteua Mudavadi kuwa Makamu Rais mwaka wa 2002 - wa kwanza kushikilia wadhifa huo katika jamii hiyo - alipingwa vikali na Michael Kijana Wamalwa wa Ford-Kenya. Wamalwa alishinda Musalia na Uhuru Kenyatta katika uchaguzi kuwa Makamu Rais wa nane. Wamalwa alifariki Agosti 2003, na ingawa Rais Mwai Kibaki alimteua mwingine kutoka jamii yake kuchukua nafasi yake - Moody Awori – hatua hiyo ilipingwa na wenzake kutoka Kaunti za Bungoma na Trans Nzoia. Musikari Kombo, ambaye alichukua nafasi ya Wamalwa kama kiongozi wa chama cha Ford-Kenya, aliongoza malalamishi kwa Kibaki akisema walitaka Makamu Rais ateuliwe kutoka kaunti hizo mbili na kutoka chama cha Ford-Kenya.

Awori, anayetoka Kaunti ya Busia, alikuwa mwanachama wa chama cha Raila cha Liberal Democratic Party (LDP). Mgogoro huo ulikuwa sawa na vita vya ubabe wa kisiasa vilivyoshuhudiwa miaka ya sabini na themanini kati ya Masinde Muliro na Moses Mudavadi, ambaye alikuwa waziri wa serikali za wilaya mwenye nguvu katika serikali ya Moi.

Nyota za wanasiasa waliokuwa na ushawishi wakati huo, akiwemo Mbunge wa Butere, Martin Shikuku na mwenzake wa Kimilili, Elijah Mwangale, pia zilikosa kung'aa katika ngazi ya kitaifa. Kwa mfano, Shikuku aligombea urais 1997 kwa chama cha Ford Asili na akapata kura 36,302 ambazo zilikuwa asilimia 0.60 ya kura zilizopigwa.

Ingawa ni wengi, Dkt Wabwire anasema viongozi wa kisiasa Waluhya - jamii ya pili kwa wingi Kenya baada ya Wakikuyu - kwa miongo mingi imekuwa ikikosa kuungana na kukosa mwelekeo. Kwa mfano, ingawa Mzee Mudavadi (Moses) anasifiwa kwa maendeleo, ikiwemo kutafutia kazi wakazi wa eneo hilo, Muliro alilenga umoja wa kisiasa kama njia ya kupata nguvu na ushawishi katika serikali.

Hata hivyo, Dkt Wawire anasifia uhusiano wa muda mrefu kati ya Musalia na Wetang'ula. Vinara hao wawili wa Kenya Kwanza sasa wanabeba ndoto ya kisiasa ya wakazi wa magharibi ya Kenya, ambao wanalenga macho yao kwa wadhifa wa juu zaidi nchini. Ingawa wadau wa siasa wanakubaliana kuwa mmoja wao anafaa kuwa kiongozi wa nchi, njia ya kufikia hilo inabaki kuwa chanzo cha mjadala na kutofautiana.

Kwa mfano, Wetang'ula anashikilia kuwa Waluhya wanafaa "kujinasua" kutoka kwa ushawishi wa Bw Odinga, jambo linaloelezea uamuzi wake wa kuhama uliokuwa muungano wa NASA, ulioongozwa na Bw Odinga, akaungana na Ruto. Hatua ya pili, kulingana na Wetang'ula, ni kubadilisha wafuasi wa ODM katika eneo hilo kabla ya kutafuta kuungwa mkono na Wakenya wengine.

Hata hivyo, Oparanya anachukulia kauli hizo kuwa ukosefu wa maono mapana. Anaamini kuwa, ili eneo hilo liweze kuwa na usemi kitaifa, ni lazima liungane na jamii jirani chini ya mpangilio wa zamani wa "Kavirondo" si kwa kujitenga na jamii zingine.

Kwa wakati huu, huku Musalia na Wetang'ula wakitulia katika enzi mpya ya kisiasa chini ya Ruto, waangalizi na wachanganuzi watakuwa macho kufuatilia jinsi watakavyotimiza ahadi zao za kampeni kwa wakazi wa magharibi ya Kenya na njia watakayofuata kuelekea tuzo inayomezewa mate mwaka wa 2027 na baadaye.

**Migogoro hiyo ni sawa na vita vya ubabe wa kisiasa vilivyoshuhudiwa miaka ya sabini na themanini kati ya Masinde Muliro na Moses Mudavadi. Nyota za wanasiasa wenye ushawishi mkubwa wakati huo, akiwemo Mbunge wa Butere Martin Shikuku na mwenzake wa Kimilili. Elijah Mwangale, pia hazikung'aa katika jukwaa la kitaifa.**



Moses Wetang'ula

Nation Media Group "ePaper Copy"

## SAYANSI NA TEKNOLOJIA



Simu mpya ya iPhone 14 Pro

# Kamera ya simu chapa iPhone 14 Pro ni ya ajabu

Simu mpya aina ya iPhone 14 Pro na iPhone Pro Max zina muundo mpya wa kipekee na wenye mvuto mkubwa. Ni muundo unaowapa wateja nafasi ya kufurahia muundo wa simu aina ya iPhone.

Simu hiyo ina kamera yenye ukubwa wa Megapixel 48 - kiwango cha kwanza kwenye miundo yote ya simu aina ya iPhone. Kamera hiyo ina uwezo wa kubadilisha na kuboresha picha zilizopigwa kwa kuimarisha mwonekano wake zaidi.

Muundo huo mpya unazifanya simu aina ya iPhone kuwa za maana kwenye matumizi ya kila siku katika masuala kama vile kurekodi video au mambo yanayohitaji mawasiliano ya dharura.

Simu hizo mbili zitaanza kupatikana kwa rangi nne tofauti: zambarau, fedha, dhahabu na nyeusi. Zitakuwa na urefu wa inchi 6.1 na 6.7 mtawalia.

# MBONA TURUDI MWEZINI?



Roketi isiyo na jina ya mwezini ikiwa kwenye jukwaa la kuirusha katika kituo cha shirika la Nasa cha Kennedy Space Center, jijini Cape Canaveral, jimbo la Florida, Amerika, mnamo Septemba 6. CHINI: Mwanaanga wa Amerika Stanley Glen Love akiongea na wanahabari katika kituo cha Kennedy Space Center.

WASHINGTON

MNAMO Septemba 12, 1962, aliyekuwa rais wa Amerika, John F Kennedy alitangazia Waamerika mpango wa kumtuma mtu kwa Mwezi kabla ya miaka kumi kukamilika. Huo ni wakati ambao Vita Baridi vya Dunia vilikuwa vimechacha. Amerika ilihitaji ushindi ili kudhihirisha ubabe wake kwa masuala ya angani baada ya Urusi, wakati huo ikiwa Muungano wa Mataifa ya Sovieti (USSR), kurusha setilaiti yake ya kwanza angani ikiwa na binadamu. "Tumeamua kwenda kwa Mwezi," akasema Kennedy, akihutubia umati wa watu 40,000 waliokusanyika katika Chuo Kikuu cha Rice.

"Tumekubali mtihani huo, hatuwezi kurudi nyuma na ni lazima tushinde," akasema.

Miaka sitini baadaye, Amerika inajiandaa kutuma roketi nyingine kwa Mwezi, inaiyoitwa Artemis. Lakini, je, mbona inarudia jambo ambalo tayari lishafanywa?

Katika miaka ya hivi karibuni, Amerika imekuwa ikishinikizwa na wanaanga kwenda moja kwa moja katika Sayari Mirihi (Mars). Shinikizo hizo zimekuwa zikitolewa na baadhi ya wanaanga kama Michael Collins (wa roketi ya Apollo 11) na mwanzilishi wa kampuni ya Mars Society, Robert Zublin.

Hata hivyo, Shirika la Uanaanga la Amerika (NASA) linashikilia kuwa ni muhimu kwenda kwa Mwezi kwanza kabla ya kutuma roketi katika Sayari Mars. Sababu ni hii; NASA inataka kubuni mkakati ambapo watu itakaotuma kwa Mwezi wataweza kukaa humo kwa wiki kadhaa badala ya siku chache pekee, kama ilivyofanya Roketi Apollo.

Lengo kuu ni kuelewa jinsi ya kujitayarisha kwa safari ya kwenda katika Sayari Mars, kwani itadumu kwa miezi kadhaa. Kiwango cha joto huongezeka sana katika anga za juu, hali ambayo huenda ikawa tishio la kiafya kwa watakaotumwa.

Kiwango cha joto si cha juu sana katika eneo kiliko Kituo cha Kimataifa cha Angani (ISS). Lakini hali ni tofauti katika eneo la Mwezi. Kwa kutuma Roketi Artemis mwezini, wataalamu wanalenga kubaini athari za kiwango hicho cha joto kwa viumbe walio hai. Wanalenga pia kubaini uwezo wa vazi maalumu la kudhibiti kiwango cha juu cha joto.

Ili kuepuka matumizi ya pesa nyingi kufadhili ziara hizo, NASA pia inalenga kutumia rasilimali chache ilizo nazo. Kwa



mfano, imebainika kuwa katika eneo la kusini mwa Mwezi, kuna maji ya barafu yanayoweza kugeuzwa kuwa mafuta ya roketi. NASA pia inataka kubaini ujuzi wa kitekinolojia ambao itatumia katika Sayari Mars, ikiwa utafaulu katika himaya ya Mwezi.

Tekinolojia hiyo inajumuisha mavazi mapya ya kisasa kwa wanaotumwa angani. Kazi hiyo ilipewa kampuni ya Axiom Space. Mavazi hayo yatatumiwa na watakaotumwa kwa Mwezi. Roketi itakayotumwa imepangiwa kufika mwezini kufikia mwaka wa 2025.

Mahitaji mengine: Magari - yenye hewa na yasiyo hewa ndani - ili kuwezesha wanaanga kusafiri na kutalii kikamilifu Mwezi. Mwisho, ili kupata kawi ya kutosha, kituo hicho kinabuni kifaa cha kuzalisha nishati aina ya nyuklia ambacho kitakuwa katika roketi hiyo.

Itakuwa rahisi kusuluhisha changamoto zitakazoibuka mwezini, kwani ni safari ya siku kadhaa, ikilinganishwa na Sayari Mars, ambayo inachukua miezi kadhaa kuifikia.

Nguzo kuu ya mpango wa kurusha Roketi Artemis ni kubuniwa kwa kituo maalumu cha angani karibu na Mwezi, kinachoitwa Gateway.

Kituo hicho kitatumiwa kama kiunganishi na chombo cha mawasiliano kabla ya ziara ya kwenda Mars.

Mbali na kujiandaa kwenda Mars, Waamerika wanataka kwenda mwezini kabla ya Wachina, ambao wanapanga kuwatuma wanaanga wao ifikapo mwaka 2030.

China ndiyo mshindani mkuu wa Amerika katika masuala ya angani. Hii ni ikizingatiwa kuwa Urusi haijawa ikituma wanaanga angani kama awali. "Hatutaki China ifike huko na kuanza kujigamba kwa kusema: "Hii ni himaya yetu," akasema kiongozi wa NASA, Bill Nelson.

Kinyume na Roketi Apollo, iliyofanikiwa kuleta kilo 400 za mawe kutoka mwezini, Roketi Artemis inatarajiwa kukusanya maelezo ya kina kuhusu hali ilivyo mwezini. "Sampuli tulizookota wakati wa ziara ya Roketi Apollo ilibadilisha dhana zetu kuhusu mpangilio wa anga," akasema mwanaanga Jessica Meir, kwenye mahojiano na shirika la AFP. "Nadhani tuna matarajio makubwa kwa mpango wa Artemis pia," akaeleza.

Anatarajia mafanikio makubwa ya kisayansi kutokana na ziara hiyo.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya Afrika

■ VIONGOZI WAAHIDI KUIMARISHA USHIRIKA



Rais William Ruto alifanya mazungumzo na Rais wa Somalia Hassan Sheikh Mohamud katika Ikulu ya Nairobi mnamo Septemba 22. Walizungumzia hali ya usalama Somalia na Upembe wa Afrika. PICHA | PSCU

# UHUSIANO MPYA NA SOMALIA

*Uhasama katika Mohamud na Farmaajo umefufuliwa huku Somalia ikikumbatia utawala wa Ruto baada ya nchi hizo mbili jirani kuwa na uhusiano mbaya katika miaka ya hivi majuzi. Mohamud amekuwa mwepesi kumkubali kiongozi mpya wa Kenya. Alikuwa miongoni mwa viongozi wa nchi kadhaa za Afrika ambao walituma risala za pongezi kwa Dkt Ruto hata kabla ya ushindi wake kuthibitishwa na Mahakama ya Upeo.*

• NA OSCAR OBONYO

Kuchaguliwa kwa William Samoei Ruto kuwa Rais wa tano wa Kenya kulisababisha sherehe kubwa nchini Somalia, sawa na Nairobi. Tabaka la kisiasa nchini Somalia lina matumaini sawa na mpiga kura Kenya.

Ahmed Ali Salaah, ambaye ni mshauri wa masuala ya Teknolojia ya Habari (IT) jijini Nairobi, asili yake ikiwa Garowe, jimbo la Putland, anasema wafuasi wa aliyekuwa rais wa Somalia, Mohamed Farmaajo, wanasherehekea kutokana na "uhusiano wa kisiasa" kati yake na kambi ya Dkt Ruto.

Mantiki ya kauli ya Salaah ni kwamba Farmaajo anaweza kutumia uhusino wake na serikali ya Ruto kutekeleza jaribio lake la kurudi mamlakani.

Hivyo ndivyo Rais wa sasa Hassan Sheikh Mohamud alifanya kurudi mamlakani miezi mitatu na nusu iliyopita.

Huku akitambua kuwepo kwa ushirika wa kisiasa kati ya Dkt Ruto na Farmaajo, Rais Mohamud amechukua hatua ya haraka na kumkubali Ruto.

Ndiyo maana alikuwa miongoni mwa viongozi wa kwanza Afrika kutuma risala za pongezi punde tu Ruto alipotangazwa mshindi wa uchaguzi mkuu wa Agosti 9, hata kabla ya ushindi huo kuidhinishwa na Mahakama ya Upeo.

Kenya ni kituo muhimu ambako wanasiasa wa Somalia hupanga mikakati yao ya kisiasa. Kwa wanasiasa hao, hasa wamegombea urais na ubunge, Nairobi imekuwa kituo muhimu kwao kushirikisha shughuli zao za kampeni. Familia za wengi wao pia zinaishi na kusoma humu nchini, hasa jijini Nairobi.

Wakiwa Kenya, Salaah anasema, wanasiasa wa Somalia hufaidi kutokana na wataalamu katika nyanja mbalimbali kama uanahabari, mawasiliano, IT, utafiti na huduma za tafsiri kutoka lugha ya Kisomalia hadi Kizungu.

...Endelea Uk 26

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Afrika

# Ushirika mpya wa Nairobi na Mogadishu



Wanajeshi wa Kenya chini ya mpango wa Umoja wa Afrika nchini Somalia wakipiga doria mjini Kismayu mnamo Novemba 22, 2015.
PICHA I JEFF ANGOTE

...Kutoka Uk 25

Farmaajo, ambaye tayari ametangaza kumpinga Mohamud katika uchaguzi wa urais wa 2026, anaelewa vyema umuhimu wa Kenya.

Kabla ya kumshinda Mohamud mnamo 2016, Farmaajo alikuwa akizuru Nairobi kila mara kupanga kampeni zake na kuchangisha. Aliongoza mikutano katika mikahawa mbalimbali ya kifahari jijini.

Kiongozi wa chama cha Wadjir Abdirahman Abdishakur, ambaye zamani alikuwa mwandani wa Farmaajo, pia aliendesha shughuli zake za kisiasa jijini Nairobi kupanga njama ya kuondolewa mamlakani kwa Farmaajo.

Hata hivyo, mnamo Agosti 2018, serikali ya Kenya ilifutilia mbali mkutano wa kisiasa wa Abdishakur jijini Nairobi uliopangwa na aliyekuwa Kiongozi wa Wengi katika Bunge la kitaifa Aden Duale.

Kenya ilisema haingeruhusu "kiongozi wa upinzani nchini Somalia kuhujumu serikali yao iliyochaguliwa kidemkrasia katika ardhi yetu."

Leo, masilahi ya wanasiasa wa Somalia nchini Kenya ni sawa na yalivyokuwa awali. Msisimko miongoni mwa wafuasi wa Farmaajo unatokana na hali kwamba kiongozi huyo wa zamani wa Somalia ni mshirika wa karibu wa Bw Duale.

**Mohamud ndiye alikuwa mamlakani Somalia iliposhtaki Kenya katika Mahakama ya Kimataifa kuhusu Haki mnamo 2014. Ndiye kutatua mzozo kuhusu mpaka baharini ulioleta uhasama kati ya mataifa hayo mawili.**

Wawili hao wanatoka ukoo mkubwa wa Darod.

Akiongea na kituo cha habari cha Amerika (CNN) baada ya ushindi wake kuthibitishwa na Mahakama ya Upeo, Dkt Ruto aliahidi kushirikiana na mwenzake wa Somalia "kuimarisha ujirani mwema na kuimarisha usalama."

Naye Waziri wa Habari Somalia, Daouf Aweys, akihutubia wanahabari jijini Nairobi, alisema Rais Mohamud na Rais Ruto wanalenga kuimarisha uhusiano kati ya mataifa hayo mawili. Waziri huyo aliondoa hofu ya kuwepo kwa hali ya kutoelewana kati ya mataifa hayo mawili.

Awey pia aliondoa hofu kuhusu uwezekano wa uhasiano huo kudhoofika baada ya Dkt Ruto kushika usukani.

"Makubaliano yoyote yaliyofikiwa kati ya mataifa haya mawili yatasalia. Kama kuna masuala tata, tutabuni kamati maalumu kuhakikisha yanasuluhishwa."

Hakikisho la Waziri Aweys ni muhimu ikizingatiwa kuwa kulitokea mkwaruzano kati ya kambi za Ruto na mtangulizi wake Uhuru Kenyatta. Bw Duale ametekeleza wajibu mkubwa katika uhusiano kati ya Kenya na Somalia, kwa misingi kuwa amewahi kushikilia wadhifa wa Kiongozi wa Wengi katika Bunge la Kitaifa kabla ya kukosana na Bw Kenyatta.

Kando na hayo, Duale, ambaye ni Mbunge wa Garissa Mjini, anatoka jamii pana ya Somalia. Alipowasili nchini Jumatatu siku moja kabla ya Dkt Ruto kuapishwa, Rais Mohamud alipokewa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA) na Bw Duale, ambaye ni mshirika wa karibu wa Rais Ruto.

Kwa kuzingatia mahusiano ya kihistoria, kitamaduni, kilugha na kibiashara, Duale anaamini uhusiano bora kati ya Somalia na Kenya utasadia kupalilia amani katika kanda hii.

**Mkataba wowote ambao mataifa hayo mawili yalitia saini utadumishwa. Ikiwa kuna masuala tata, tutabuni kamati maalumu kuhakikisha yanasuluhishwa.**

Rais wa Habari wa SomaliaDaoud Aweys

Tayari, Mohamud amezindua sera mbalimbali zinazolenga kuimarisha uhusiano kati ya Somalia na Kenya, ikiwemo kufunguliwa kwa soko la miraa nchini Somalia na kuanzishwa tena kwa safari za ndege ya Kenya Airways miezi miwili iliyopita.

Aidha, Rais Mohamud ameamuru kuondolea kwa masharti magumu ya utoaji visa vya usafiri kutoka Kenya hadi Somalia

Haya na mengine ni miongoni mwa makubaliano ambayo Rais Mohamud alitia saini na Rais Kenyatta alipozuru nchini siku 40 baada ya kuchukua mamlaka.

Kenya na Somalia pia zimeonyesha kujitolea katika kupambana na ugaidi. Kurudi kwa Mohamud na kasi yake ya kupalilia uhusiano kati ya Somalia na Kenya, ulioharibiwa na mzozo kuhusu mpaka majini, bila shaka kunaleta matumaini. Hatua hiyo imetuliza hataruki kati ya mataifa hayo mawili na kutoa nafasi kwa Meja Jenerali (mstaafu) Thomas Chepkuto, kuingia afisini Ijumaa iliyopita kama balozi mpya wa Kenya nchini Somalia. Awali, nchi hizi mbili zilikuwa zimekatiza uhusiano wa kidiplosia.

Sababu kadhaa, zikiwemo hatua ya Kenya kuendelea kushirikiana kisiasa na maafisa wa serikali ya jimbo la Somaliland na serikali ya eneo la Jubaland, zimechangia kuzorota kwa uhusiano kati ya Somalia na Kenya.

Mohamud, ambaye hatamu yake ya kwanza kama rais wa Somalia ilidumu kati ya 2012 na 2017, amekuwa na uhusiano mzuri na Bw Kenyatta ambaye pia aliingia afisini mara ya kwanza mnamo 2013.

Kinyume na Kenyatta, Mohamud alishindwa na Farmaajo mnamo katika uchaguzi wa 2017. Hatua ya Dkt Ruto na Mohamud kuahidi kushirikiana ni ishara kuwa uhasama kati ya Somalia na Kenya umepungua.

Mohamud alikuwa mamlakani Somalia iliposhtaki Kenya katika Mahakama ya Kimataifa kuhusu Haki (ICJ) mnamo 2014. Ndiye anayefaa kuondoa kitendo hicho kilichozua uhasama kati ya mataifa hayo mawili.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Dunia

HATIMAYE UHURU UMEPATIKANA

# AH, FURAHA YA UKOMBOZI

*Vikosi vya wanajeshi wa Ukraine vimepiga hatua, na wanajeshi wa Urusi wameondoka haraka - kutoka maeneo muhimu katika jimbo la Kharkiv. Wamepoteza miji ya Kupiansk, kituo muhimu cha vifaa na Izyum, walichotumia kuanzisha mashambulizi*



Mwanamume akiendesha baiskeli katika eneo la Kharkiv, mnamo Septemba 10. Kasi ambayo wanajeshi wa Ukraine wamejibu mashambulizi ya Urusi na eneo kubwa ambalo wamekomboa imeshangaza wakazi na raia wengi wa Ukraine. PICHA | AFP

• KYIV

Uso wa Natalia unang'aa anapokumbuka dakika aliyopata ukombozi wake - wakati wavamizi waliochukiwa walilazimishwa kuondoka kijiji chake, Novovoznesenske, jimbo la kusini la Kherson.

Alikuwa akiendesha kilimo hapo kwa amani na utulivu hadi wanajeshi wa Urusi walipofika Machi 29. Kile ambacho hawakuharibu walipora, anasema, vikiwemo vijiko na uma, na viatu kutoka kwa mzee aliyestaafu.

"Walikuwa wengi na wasumbufu," anasema, huku akizungusha mikono akikumbuka masaibu yake. Uhuru ulijiri Septemba 2. "Wanajeshi wetu walipofika, tulikuwa eneo la chini ya jengo," anasema mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 50.

"Waliuliza kwa lugha yetu ya Ukraine. 'kuna yeyote aliye hai?' na nikabaini walikuwa wetu. Walikuwa na maumbile mazuri wakilinganishwa na wavamizi. "Sikujua niwafanyie nini - Niwakumbatie au nishike mikono yao. Niliwagusa na nilifurahi sana."

Baada ya miezi ya mapigano, wanajeshi wa Ukraine na Urusi, wanakabili ukweli mpya. Ghafla kuna mabadiliko katika mzozo mkubwa zaidi Ulaya tangu Vita vya Pili vya Dunia.

Vikosi vya wanajeshi wa Ukraine vimepiga hatua, na wanajeshi wa Urusi wameondoka haraka - kutoka maeneo muhimu katika jimbo la Kharkiv. Wamepoteza miji ya Kupiansk, kituo muhimu cha vifaa na Izyum, walichotumia kuanzisha mashambulizi. "Jeshi la Urusi linaharakisha kupata umaarufu kama jeshi lenye mbio zaidi ulimwenguni," Andriy Yermak, mkuu wa wafanyakazi wa Rais Volodymyr Zelensky, aliandika katika Twitter. "Waendelee kukimbia."

Mitandao ya kijamii hapa imefurika picha za

...Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Dunia

# Ukraine: Furaha kwa vijiji kukombolewa



Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, akizuru maeneo ya vita na waasi wanaoungwa mkono na Urusi katika eneo la Donetsk kuadhimisha Siku ya Vikosi vya Ulinzi vya Ukraine mnamo Disemba 6, 2021.

**2000**

Rais Zelensky anasema wanajeshi wamekomboa karibu kilomita 2,000 mraba tangu mwanzo wa Septemba.

..Kutoka Uk 27

maeneo yaliyoharibiwa au kuachwa na wanajeshi wa Urusi na wale wa Ukraine wakipeperusha bendera katika maeneo mapya waliyokomboa.

Kasi na upana wa makabiliano dhidi yao zimeshangaza wavamizi na raia wengi wa Ukraine. "Tulihitaji ushindi mkubwa kutuchangamsha," anasema, "na inaonekana kuna ufanisi katika Kharkiv. Lakini bado wako na silaha na majeshi na wameteka sehemu kubwa ya nchi yetu. Watu bado wanajua majirani wetu ni akina nani. Lakini hofu imepungua na imani imeongezeka."

Ufanisi huo umeipa nguvu nchi hiyo iliyoharibiwa na vita, baada ya kushindwa vibaya katika jimbo la Donbas. Tuliporipoti kutoka hapo mnamo Juni, hapakuwa na ishara wanajeshi wa Ukraine wangeweza kutekeleza pigano kali. "Ni muujiza wa kijeshi," anasema Mykhailo, mhandisi wa IT mwenye umri wa miaka 38.

"Muujiza huo umefikiwa kupitia silaha nyingi kutoka nchi za kigeni - yakiwemo makombora makubwa ya masafa marefu - na ujasusi kutoka nchi za nje.

> **Tulihitaji ushindi mkubwa kutuchangamsha, na inaonekana kuna ufanisi katika Kharkiv. Lakini bado wako na silaha na majeshi na wameteka sehemu kubwa ya nchi yetu.**
>
> Andriy Yermak, mkuu wa wafanyakazi wa Rais Volodymyr Zelensky

**Inaonekana kama wanajeshi wa Ukraine waliwashinda maarifa wale wa Urusi, sio kwa mara ya kwanza, kwa kuzungumzia mipango ya kukabiliana jimbo la kusini la Kherson.**

Aidha, inaonekana wanajeshi wa Ukraine waliwashinda maarifa wale wa Urusi, kwa kuzungumzia mipango ya kuwakabili katika jimbo la kusini la Kherson.

Inaonekana Urusi ilimeza chambo, kwa kutuma wanajeshi huko, na kuacha maeneo waliyokalia katika Kharkiv na kujiweka katika hatari. Makabiliano hayo pia yameonyesha wanajeshi wa Ukraine wanaweza kushinda wale wa Urusi katika uwanja wa vita, kulingana na wataalamu wa kijeshi wa nchi za Ulaya na Amerika.

"Sasa tunaona wanajeshi wa Urusi wakishindwa, si kushindwa tu, ni kuwezwa," anasema Profesa Michael Clarke, aliyekuwa Mkurugenzi wa taasisi ya Royal United Services Institute. Anaona haya kama "mabadiliko ya mapema".

Juzi, Rais Zelensky alisema wanajeshi walikuwa wamekomboa kilomita 2,000 mraba tangu mwanzo wa Septemba. Jeshi lilisema ni kilomita 3,000 mraba.

Kwa wakati huu, wanahabari hawaruhusiwi kuingia maeneo ambako vita vimechacha. Hatuwezi kuthibitisha madai ya Ukraine. Urusi inakiri kuwa wanajeshi wake wameondoka sehemu za Kharkiv, ikisema "waliwekwa pamoja" na sio kutimuliwa.

Licha ya hatua ambazo Ukraine imepiga majuzi, wanajeshi wa Urusi wameteka asilimia 5 ya Ukraine - likiwemo jiji la Kherson. Lilikuwa jiji la kwanza muhimu la Ukraine kutekwa.

Tulifaulu kumfikia mwanamke ambaye bado anaishi huko - anayesema wanajeshi wa Urusi wameanza kujificha. Kwa usalama wake, hatutataja jina lake.

"Kwa siku mbili au tatu zilizopita, jeshi linaonekana kutulia kidogo," anatueleza. "Hawaonekani sana katika mikahawa. Vita vikianza barabarani, itakuwa hatari sana. Lakini nitajificha siku kadhaa au wiki nikiweza. Nataka kuona wanajeshi wetu hapa kuwashukuru. Nataka kuona ushindi."

Wengine wanaosubiri ushindi ni kundi la wanaharakati walio ndani ya jiji hilo, ambao wanapinga wanajeshi wa Urusi. Wanakusanya habari za kijasusi na kuwapa wanajeshi wa Ukraine. Mwanachama wa kundi hilo - ambaye hatuwezi kumtaja jina - alitwambia wanawindwa.

"Wanajeshi wa Urusi wanatafuta maeneo ambayo picha zinapigwa," anasema. Kuna misako mikubwa katika majengo yaliyo katika vituo muhimu.

Kumekuwa na visa viwili wiki iliyopita vya watu kutolewa barabarani." Lakini anasema habari kutoka maeneo ambako vita vimechacha zinaleta matumaini. "Watu sasa wamepata nguvu kutokana na ushindi eneo la Kharkiv," akatwambia. "Watu wengi wana matumaini kuwa ndio watafuatia,"

Jiji la Kherson litakuwa la vita vijavyo, lakini kufikia sasa, hatua zinazopigwa na jeshi la Ukraine ni afueni kwa Ukraine na nchi za Magharibi zinazoiunga mkono. Ufanisi huo ukidumishwa, mzozo unaweza kubadilika. Hakuna anayetarajia Rais Putin kusalimu amri. Ikiwa ni Ukraine, ana maoni tofauti. Lakini katika uwanja wa vita wanajeshi wa Urusi wamevurugika na kutoroka. Huko si kushindwa tu. Ni kuaibishwa.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Dunia

■ MAUZO UGENINI YALIONGEZEKA KWA ASILIMIA 15 MWAKA ULIOPITA

# UTAMADUNI THABITI WA SIGARA CUBA

*Kampuni ya Cuba iliyosokota sigara za Castro ingali inajitahidi kutengeza "sigara bora zaidi." Sigara chapa Cohiba Lancero, aliyokuwa akivuta hadi alipoacha uvutaji sigara mnamo 1985 akiwa na umri wa miaka 59, bado inaundwa nchini humo.*



Mfanyakazi akipakia sigara katika kiwanda cha Cohiba, jijini Havana, Cuba, mnamo Septemba 8. PICHA NDOGO: Rais wa Cuba Fidel Castro, akivuta sigara wakati wa mkutano na wanahari katika uwanja wa ndege wa Jose Marti, jijini Havana, mnamo Januari 15, 1976.

● HAVANA

Akiwa ameketi mbele ya mashine inayotumika kupima ubora wa sigara, Orquidea Gonzalez anasema anajivunia kuendeleza utamaduni huo na kuchangia katika sekta ya uzalishaji wa mapato ya kigeni ambayo imekua pakubwa katika msimu wa janga la Covid-19.

"Napenda kuunda sigara." Hapa ndipo nimeishi miaka mingi, na kwangu ni sanaa. Si kila mtu anayejua kuunda sigara, sawa na ilivyo kwamba si kila mtu anayejua kuchora picha," anasema mfanyakazi huyo mwenye umri wa miaka 55.

Kazi yake ni kupima, kupitia mrija uliotengezwa kwa chuma, mvuto wa kila sigara ili kuhakikisha mvutaji sigara anapata mvuto bora. "Kama ni chini ya 40, kiwango cha mrija kimepita kiasi; ikiwa ni zaidi ya 80, kiwango kiko chini mno," akafafanua huku macho yake yakiwa yamekwama kwenye sindano ya mashine hiyo.

Kiwanda cha El Laguito kilifunguliwa mnamo 1966 eneo la Havana Magharibi kuunda sigara zilizopendwa na shujaa wa mageuzi ya Kikomunisti 1959, na rais wa muda mrefu, Fidel Castro.

Kampuni hiyo ndiyo chimbuko la sigara aina ya Cohiba, ambazo ni za kifahari zaidi nchini Cuba. Jina hilo la sigara linaashiria jinsi wenyeji asilia wa jamii ya Taino walivyoita usokotaji wa matawi ya tumbaku waliyokuwa wakivuta.

Sigara aliyoipenda sana Castro,

**Licha ya janga la corona, kiwango cha sigara za Cuba zilizouzwa katika mataifa ya kigeni kiliongezeka kwa asilimia 15 mnamo 2021, na kufikia jumla ya $568 milioni (karibu Sh68 bilioni), kulingana na shirika la Habanos S.A., linalojumuisha bidhaa zote nchini.**



Cohiba Lancero, ambayo alivuta hadi alipoacha kuvuta mnamo 1985, akiwa na umri wa miaka 59, bado inatengezwa katika kiwanda hicho.

"Licha ya changamoto zote tunazokumbana nazo, shabaha yetu ni kuunda "karibu bidhaa milioni mbili" za sigara mwaka wa 2022, au karibu 9,000 kwa siku," anasema mkuu wa kiwanda hicho, Oscar Rodriguez.

Licha ya janga la corona, kiwango cha sigara za Cuba zilizouzwa katika mataifa ya kigeni kiliongezeka kwa asilimia 15 mnamo 2021, na kufikia jumla ya $568 milioni (karibu Sh68 bilioni), kulingana na shirika la Habanos S.A., linalojumuisha bidhaa zote nchini.

Kiwanda hicho "hakikusitisha shughuli zake hata siku moja" wakati wa mkurupuko wa Covid-19, hatimaye sigara zikiibuka kuwa "bidhaa za pili zinazoongoza kwa wingi wa mapato ya kigeni nchini humo," akasema Rodriguez.

Uhispania, China, Ujerumani, Ufaransa na Uswizi ni miongoni mwa wanunuzi wakuu.

Huku wakiwa wamekamata kwa ustadi wa hali ya juu visu na gundi inayonata, mamia ya wafanyakazi wanamalizia uundaji wa ncha za sigara mpya zilizokwisha kusokotwa.

Asilimia 60 ya wafanyakazi ni wanawake – kwa kufuata utamaduni katika kiwanda hicho ulioanzishwa na Celia Sanchez, mwanajeshi mwenza wa Castro – unaolenga kuwapa fursa kina mama wasio na waume au wanawake walio na matatizo mbalimbali.

Caridad Mesa, ambaye sasa ana umri wa miaka 55, alianza kufanya kazi katika El Laguito kama msafishaji. Miaka 30 baadaye, ni msimamizi wa idara inayohakikisha sigara hazina dosari yoyote ile.

Ni muhimu kudhibiti "ubora, uzito, urefu. . .upana," anasema huku akikagua pakiti zilizopakiwa sigara chini ya picha kubwa ya shujaa wa mageuzi ya Kikomunisti Ernesto "Che" Guevara.

Sigara aina ya Cohiba, zinaweza kuuzwa kwa dola $30 (karibu Sh3,600) hadi $200 (karibu Sh24,000) kwa kila msokoto, nchini Cuba na katika mataifa ya kigeni.

"Tumbaku ya Cuba inatofautiana na aina nyingine zote kutokana na ladha ya ardhi ya Pinar del Rio," anasema Gonzalez.


Ni huko, anaongeza, "ambako mazao bora zaidi ya tumbaku hukuzwa."

Nation Media Group "ePaper Copy"

TANZIA

USHINDI DHIDI YA VIKWAZO TELE

# MWISHO WA SMAKU WA KIBIASHARA



Nation Media Group "ePaper Copy"

*Licha ya kukosa elimu rasmi, Mzee Samwell Ng'etich alifanikiwa kujenga biashara kubwa na umaarufu wa kisiasa uliowapa motisha wote aliotangamana nao.*

- Na VITALIS KIMUTAI

KIFO cha Mzee Samwell Kipterer Ng'etich kilifunga ukurasa wa mtu aliyepata mafanikio kutoka kwa ufukara mkubwa, hadi kuwa miongoni mwa wafanyabiashara maarufu na wenye ushawishi mkubwa sana.

Alikuwa amewekeza katika sekta za ujenzi, uchukuzi, kilimo cha majanichai, hoteli, uchimbaji madini, mabohari ya kuwekea bidhaa na maduka.

Kifo chake pia kiliwezesha nchi kufahamu kuhusu maisha ya mtu ambaye, licha ya kuachia masomo Darasa la Tatu katika Shule ya Msingi ya Keongo, alihudumu kama diwani (kabla na baada ya ugatuzi) na Naibu Meya wa mji wa Kericho. Alijiunga na shule hiyo mnamo 1956.

Marehemu alizaliwa katika kijiji cha Chepsetyon, Kaunti ya Kericho, mnamo 1949. Alifariki akitibiwa ini katika Hospitali ya MP Shah, Nairobi, wiki chache baada ya kurudi nchini kutoka India, alikokuwa amepelekwa kwa matibabu maalumu. Alikuwa na umri wa miaka 73.

Mzee Ng'etich alifahamika kama "Chepsetyon" (jina la kijiji alikotoka). Alikuwa na upekee wake kutokana na mavazi aliyovaa. Alikuwa na mazoea ya kuvaa suti aina ya 'Kaunda' na shati za maua.

Aliweka nywele yake kwa mtindo wa 'Afro.' Hadithi yake ni ya mtu aliyetajirika licha ya kuzaliwa katika umaskini. Baada ya kuacha shule, Ng'etich alifanya kazi kadhaa za vibarua ikiwemo kuchimba vyoo, kupalilia mahindi, kuchuma majanichai, kuuza kuku na kwenye hoteli kama mhudumu. Badaye alifungua hoteli yake, baa na duka. Muda si mrefu, alijitosa kwenye biashara ya matatu.

Baadhi ya kampuni alizoanzisha ni viwanda ya majanichai vya Mbogo Valley, Sangalo na Kuresoi; Kampuni ya Ujenzi na Uchimbaji madini ya SABS, Mabohari ya ABSS na Kampuni ya Sukari ya West Valley. Zote zilikuwa chini ya kundi la Kampuni za Kipchimchim.

**1949**

Alizaliwa katika kijiji cha Chepsetyon, Kaunti ya Kericho, mnamo 1949 na alifariki akitibiwa ini katika Hospitali ya MP Shah, Nairobi.

**Ng'etich alifanya kazi kadhaa za vibarua ikiwemo kuchimba vyoo, kupalilia mahindi, kuchuma majanichai, kuuza kuku na kwenye hoteli kama mhudumu. Badaye alifungua hoteli yake, baa na duka. Muda si mrefu, alijitosa kwenye biashara ya matatu.**

Licha ya mafanikio yake makubwa, familia na marafiki wake wanamkumbuka kuwa mtu mnyenyekevu na mkarimu, aliyekuwa akiwalipia karo ya shule wanafunzi zaidi ya 5,000 kutoka familia maskini. Licha ya changamoto alizokumbana nazo, hakukubali kiwango chake duni cha masomo kiwe kikwazo katika kutafuta uongozi.

Daima, alikuwa akitenga muda kumsikiliza kwa makini kila mmoja aliyezungumza naye. Alitajwa na wengi kuwa 'maktaba tembezi' kuhusu masuala yanayohusu mji wa Kericho.

Akiwa diwani wa Kapkugerwet, alifuata kwa makini vikao vya Bunge la Kaunti.

Hakusita kumrai Spika wa bunge hilo, Bw Kiptergech Mutai, kumfafanulia masuala ambayo hakuyaelewa. "Ni mzee aliyekuwa na ufahamu mkubwa wa masuala mengi. Alichukulia masuala ya wapigakura kwa uzito na alijitolea sanakubadilisha maisha ya watu aliowaakilisha," akaeleza Bw Mutai.

Ni kauli inayoungwa mkono na Bw Jackson Kikwai, aliyehudumu kama diwani pamoja na marehemu kati ya 2013 na 2017. "Mzee Ng'etich alikuwa mwenye ufahamu mpana kuhusu masuala ya kitaifa na kimataifa kuliko sisi tuliosoma zaidi yake. Tulipozuru katika mataifa ya Israeli na Namimbia kuona jinsi yalivyostawisha sekta ya kilimo, alitushangaza sana kutokana na ufahamu wake mkubwa kuhusu masuala ya tekinolojia," akasema Bw Kikwai.

Kabla ya kuondoka Kenya kuelekea Namimbia, Mzee Ng'etich alikuwa amewaonya madiwani wenzake kuwa hawangepata soko la majanichai nchini humo kwa sababu hayatumiwi kwa wingi.

Wengi walipuuza kauli yake lakini hatimaye ikawa ya kweli. Aliyekuwa Meya wa Kericho, Bw Joel Siele, anaeleza kupendezwa na imani kubwa aliyokuwa nayo Mzee Ng'etich kwa mipango yote aliyokuwa nayo.

"Hakukata tamaa kwa lolote alilofanya. Kila mpango wake ulipokosa kufaulu, alikuwa akijipanga na kuanza tena. Watoto wake walimuunga mkono katika biashara zake. Wanazisimamia vizuri sana. Wamekuwa mfano bora kuhusu jinsi familia inafaa kusimamia na kuendesha biashara zake kwa umoja," akasema Bw Siele.

Kando na biashara, Bw Ng'etich pia aliwafunza watoto wake jinsi ya kufanikiwa maishani. "Alikuwa mfano bora wa jinsi mtu anaweza kufuata ndoto zake na kufaulu maishani," akasema mwanawe, Ben Soi.

Akaongeza: "Alizuru mataifa mengi yakiwemo China, Dubai, India, Namimbia, Uingereza na Israeli. Hakuna lolote linalomtisha, hata vikwazo vya lugha."

Ingawa ametuacha, maisha ya Mzee Ng'etich ni mfano bora wa jinsi mtu anaweza kufanikiwa maishani bila kujali asili yake ama changamoto alizokumbana nazo mwanzoni.

*nenyonn@gmail.com*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KENYA TOP 100 MID-SIZED COMPANIES Business Daily KPMG

# EVOLVE

## BECAUSE YOUR BUSINESS DOESN'T STAND STILL – IT EVOLVES

Each stage of your business cycle presents its own set of opportunities and challenges. Do you have what it takes to be successful at each stage? Enter the 2022 Top100 Midsized Companies Survey and take your seat among the great.

**Benefits:**

- Recognition for companies that have successfully redefined their business and remained agile in an increasingly uncertain business landscape.
- Access to an industry benchmarking report and thought leadership to all participating companies.
- Opportunities to network with peers and sponsors through the exclusive Top100 Mid-Sized Companies conference and gala dinner.
- Winners will be eligible to use the 2022 Kenya Top100 Mid-Sized Companies Club logo.

Survey closes on 9 September 2022


**Submit your entry at: www.eastafricatop100.com**

**Kenya100@kpmg.co.ke**

**020 280 6000**







**Be seated among the great.**

Business Daily KPMG

In partnership with:

IFC International Finance Corporation WORLD BANK GROUP
*Creating Markets, Creating Opportunities*

#Top100KE Top100SME @Top100SME

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep




SMS the word **GAZETI** to **20567**,
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE** SMS text and **FREE** Delivery

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*